TOLEO NAMBA: 03 | JUNI 2023

# JARIDA LA FILMIKA

*Filamu ni biashara, Filamu ni ajira*

**Mama ni Mama**
UKURASA - 13

**Mjue Msanii wako**
UKURASA - 28

**Kona ya mashabiki**
UKURASA - 51


Seko Shamte


Gabo Zigamba


Hidaya Njaidi


Idris Sultan



# YALIYOMO








Neno kutoka kwa Katibu Mtendaji ........................................................ 3

Bodi ya uhariri ........................................................................................ 5

Mama ni Mama ..................................................................................... 13

Miaka 24 ya Hidaya Njaidi ................................................................... 20

Picha na matukio .................................................................................. 21

Seko Shamte .......................................................................................... 22

Mjue Msanii wako ................................................................................ 28

Tuzo za filamu ...................................................................................... 30

Wapambaji ............................................................................................ 46

Ushirikiano wa wasanii ........................................................................ 49

Kona ya mashabiki ................................................................................51

Chanzo na Historia ya Majina .............................................................. 53






## Kutoka kwa Katibu Mtendaji

### Dkt. Kiagho Kilonzo

Sekta ya Filamu ni kiwanda chenye fursa zinazoweza kuchangia kwenye uchumi wa nchi, hususan katika uzalishaji wa ajira na mchango katika pato la Taifa. Pato litokanalo na kazi za filamu duniani linakadiriwa kuzidi dola za kimarekani Bilioni 2.2. Hapa Tanzania, kampuni za ndani zinazoandaa filamu (Film Producers) zilikuwa 94 mwaka 2022 idadi hiyo ikiwa ni ongezeko kutoka kampuni 4 miaka ya 1960.

Hivi sasa Sekta ya Filamu nchini inakadiriwa kuwa na zaidi wadau Milioni Moja (pamoja na familia zao) wanaoitegemea kimaisha. Ongezeko hilo la Kampuni za uandaaji wa filamu hapa nchini umeenda sambasamba na ukuaji katika eneo la uzalishaji wa filamu hapa nchini ambapo eneo hilo pekee limekuwa mara 10 zaidi kwa kipindi cha miaka kumi. Mwaka 2011 filamu zilizoripotiwa kuzalishwa zilifika 206 ambapo mwaka 2022 ziliripotiwa filamu 2044 kama inavyoonyeshwa katika Jedwali Na. 1 hapo chini.

*Jedwali Na.1: Ukuaji wa Uzalishaji wa Filamu nchini kwa kipindi cha Miaka 10*

| MWAKA | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| IDADI YA FILAMU | 206 | 414 | 1,181 | 1,339 | 653 | 706 | 762 | 832 | 1,573 | 2,044 |

Kwa upande wa usambazaji wa filamu hapa nchini, kumekuwa na mapinduzi makubwa ya kidijiti katika eneo hilo, ambapo usambazaji wa kidijiti umezidi ule wa Teknolojia ya Digital Versatile Disc (DVD) na Compact Disc (CD) iliyoanza kushamiri sana hapa nchini miaka ya 1990 na kudondoka kwa kasi (86%) mwaka 2008 baada ya kushamiri zaidi Teknolojia ya usambazaji wa filamu kwa njia ya flush disc. Hivi sasa, eneo ambalo filamu zinasambazwa zaidi kidijiti ni kwenye Runinga, na hasa kupitia visimbuzi. Kwa mfano Mwaka 2013 kulikuwa na vituo vya Runinga 23 nchini ambapo hivi sasa kuna zaidi ya vituo 56, kama Jedwali Na. 2 linavyoonyesha hapo chini.

*Jedwali Na. 2: Hali ya Usambazaji wa Filamu Nchini kupitia Runinga*

| MWAKA | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VITUO VYA RUNINGA | 23 | 25 | 25 | 25 | 27 | 30 | 37 | 44 | 50 | 56 |

Kumekuwa visimbuzi lukuki hapa nchini, jambo linalochangiwa na ukuaji wa Tteknolojia hiyo, ambapo Mwaka 2013, kulikuwa na visimbusi 74,562 ilhali kwa sasa kuna visimbuzi zaidi ya Milioni 3, kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.3 hapo chini ambapo Kampuni ya Startimes ndiyo yenye visimbuzi vingi zaidi ikifuatiwa na Azam kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.4.

*Jedwali Na. 3 Idadi ya Visimbuzi vinavyofanya kazi (active decorders) nchini*

| MWAKA | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| IDADAI YA VISIMBUZI | 74,562 | 96,823 | 125,043 | 158,224 | 158,224 | 1158,224 | 1,432,398 | 1,472,317 | 1,613,031 | 3,352,860 |

*Jedwali Na.4: Idadi ya Visimbuzi kwa kila Chombo/Mmiliki nchini Tanzania*

| Chombo | Idadi ya Visimbuzi |
|---|---|
| Star time | 2,091,263 |
| Azam | 900,867 |
| DSTV | 256,329 |
| Continental | 65,554 |
| Zuku | 34,115 |
| DiGiTek | 17,392 |
| Agape | 4,001 |
| **JUMLA** | **3,369,521** |

Aidha, pamoja na ukuaji huo lukuki, kumekuwa na changamoto ya idadi ya filamu za Kitanzania zinazoonyeshwa kwenye vituo vya runinga vya hapa nchini dhidi ya zile za nje ya Nchi. Kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), mwaka 2022, filamu ndefu (feature films) zilizoandaliwa na kampuni za hapa nchini zilionyeshwa kwa 20% tu dhidi ya zile za nje, ambazo zilionyeshwa kwa 80%. Vivo hivyo kwa Tamthilia, kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 5 hapo chini.

*Jedwali Na.5: Hali ya Uonyeshwaji wa Filamu kwenye vituo vya Luninga Tanzania*

| AINA YA MAUDHUI | MAUDHUI YA NDANI | MADHUI YA NJE |
|---|---|---|
| Filamu ndefu (Feature Films) | 20% | 80% |
| Tamithiliya (Series) | 20% | 80% |
| Makala (Documentaries) | 10% | 90% |
| Vichekesho (Commedy) | 20% | 80% |
| Vikaragosi (Cartoon) | 5% | 95% |

Uchunguzi mdogo (survey) umeonyesha kuwa sababu kubwa ilizosababisha hali hiyo ni filamu zetu kukosa mvuto kutokana na ubora hafifu wa kazi kulinganisha na zile zinazoandaliwa na kampuni za nje ya Nchi.

Ili kunusuru hali hiyo, Serikali kupitia Bodi ya Filamu Tanzania imedhamiria kuanzisha Shule ya Filamu nchini kwa kushirikiana na Asasi ya Busan Foundation for International Cooperation (BFIC) kutoka nchini Korea Kusini.

Kwa upande wa mitaji, Serikali imefufua uliokuwa Mfuko wa Utamaduni na kuongeza kipengele cha Sanaa katika Mfuko huo, ambapo Mfuko huo unatoa mitaji yenye masharti nafuu na mafunzo ili kuziwezesha kazi za wadau katika Sekta ya Sanaa na Utamaduni kukidhi vigezo vya mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Mfuko huu unatoa huduma katika maeneo ya urithi wa utamaduni, matumizi ya lugha na fasihi, sanaa za maonesho, sanaa za ufundi, utengenezaji wa filamu na makala, muziki, uandishi wa vitabu vya kukuza lugha ya Kiswahili, na miradi mingine ya kukuza Utamaduni, Sanaa na Maadili. Aidha, walengwa wa Mfuko ni watu binafsi, vikundi, vyama, mashirikisho, vituo vya elimu na mafunzo, asasi za kiraia na taasisi zinazojishugulisha na kazi za kukuza na kuendeleza kazi za Utamaduni na Sanaa.



Katika kuhakikisha kuwa mipango ya maendeleo ya Sekta ya Filamu inatekelezwa kikamilifu, uwekezaji wa rasilimali fedha ni muhimu. Hata hivyo kwa kutegemea bajeti ya ruzuku kutoka Serikalini pamoja na ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vya Bodi ya Filamu pekee hakutoshelezi.

Kwa muktadha huu, Bodi ya Filamu imeweka mpango wa kuanzisha tozo maalumu kwa watuamiaji wa maudhui za filamu (Film Levy), ambapo mapato yake yataelekezwa moja kwa moja katika shughuli za maendeleo ya Sekta ya filamu kama vile uandaaji wa kazi bora, utafiti na ukuzaji wa masoko ya bidhaa za filamu, uwekezaji katika miundombinu ya filamu, mitaji pamoja na kuongeza weledi kwa wanatasnia ya filamu.



# BODI YA UHARIRI


**MWENYEKITI**
Dkt. Kiagho Kilonzo

**MHARIRI**
Bibi. Edna Rajab

**MPIGA PICHA**
Brighton James

**WAJUMBE**
Bw. Emmanuel Ndumukwa
Bi. Martha Paul
Bw. Mustafa Hassanali

**WAANDISHI**
Nzonesta Jeckonia
Brighton James
Issa Liponda

**MSANIFU**
James Erick Kuzwa
Darianus Mtembei
Juma Mkingwa

# Maoni ya Mhariri

*Tasnia ya filamu inakwenda mbio sasa*

**Na Edna Rajab**



MWANZONI mwa miaka ya 2000, Tanzania ilikuwa ni kati ya mataifa machache ambayo yalikuwa yanajivunia uwepo wa kazi nyingi za Sanaa.

Hiyo ndiyo miaka ambayo walikuwa wanatesa magwiji wa tamthilia na maigizo kama Marehemu Mzee Majuto na Mzee Small, Pwagu na Pwaguzi ambao zama zao zilikuwa zinaishia.

Kisha kikaja kizazi cha kina Muhogo Mchungu, Bambo, Zembwela na Maksi, Kingwendu, Joti na Mpoki na hawa kina JB na Richie Mtambalike.

Baadae kikaja kizazi cha kina Kanumba, Ray, Johari, Thea na wasanii wengi ambao kuanzia mwaka 2007 hadi mwishoni mwa miaka ya 2012, waliweza kuliteka soko la filamu haswa.

Filamu zilikuwa zinapendwa sana, kila Wema, Uwoya, Wolper na mastaa wengine walikuwa wanatikisa taifa hili. Lakini ghafla mambo yalibadilika kuanzia mwaka 2015 kuja huku juu, yaani kulikuwa na miaka takribani mitano hadi sita ya kifo cha soko la filamu.

Sababu zilikuwa nyingi, ikiwemo mabadiliko ya biashara yenyewe ya filamu kutoka kuzikuta dukani zinauzwa hadi kwenye simu ya  mkononi kwa maaa ya teknolojia.

Kila msanii na mdau wa filamu akawa analalamika, wapo ambao waliachana kabisa na masuala ya filamu na kuchagua kufanya mambo mengine, watoto wa mjini wanaita 'michongo'.Lakini kuna ambao walikomaa na kutafuta suluhisho, hatimaye wakalipata na sasa wapo mbali na wameaanza kuwashika mikono wale ambao walikata tama na kubaki njiani.

Kwa kipindi cha miaka mitatu, tasnia ya filamu nchini imepiga hatua na inakimbia kwa kasi sana. Serikali ya awamu ya Sita Mhe. Dk.  Rais Samia Suluhu Hassan kuwekeza nguvu kwenye filamu pia imeongezea spidi tasnia hiyo na sasa inapepea tu kimataifa.

Kuna Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa na Utamaduni, ambao kwa mara ya kwanza kwenye uzinduzi wake ulitengewa bajeti ya kwanza ya bilioni 2.5. Kisha kuna mchakato wa kuunda sera mpya ya Utamaduni itakayoendana na Dunia ya sasa.

Hayo yote yanachangia kwa kiasi kikubwa kwa tasnia hii ya filamu kushika masoko ya Dunia, kina Idris Sultan na filamu kama Slay wanatikisa *Netfilx* huko. Binti ya Seko Shamte ikiwa filamu ya kwanza ya mwanamke kutikisa huko *Netflix.*

Haya yote ni ishara ya mwendo mzuri wa filamu nchini. Rai yangu kwa wasanii ni kuongeza ubunifu zaidi ili kuendelea kutoboa, lakini pia wasiwe wavivu wa kusoma na kujifunza vitu vipya kila siku.

# MIAKA 59 YA MUUNGANO WA TANZANIA NA MUSTAKABALI WA TASNIA YA FILAMU NCHINI

Mnamo tarehe 26 mwezi wa nne Tanganyika na Zanzibar walisherehekea miaka 59 ya Muungano ambao ulizaa jina la Taifa la Tanzania.

Miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, umeleta mambo mengi sana kwenye nyanja mbalimbali hata kwenye suala la Sanaa hasa Filamu.

Historia ya Sekta ya Ffilamu nchini inaweza kuelezewa kwa vipindi vitatu, yaani kipindi cha wakati wa Ukoloni (1880 – 1961), kipindi cha Uhuru (1961 – 1990) na kipindi cha Soko Huria (1990 hadi sasa).

Bodi ya Filamu Tanzania ni Taasisi iliyoanzishwa kwa Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya mwaka 1976.

Sheria hiyo ina Kanuni zake zilizotolewa kwa Tangazo la Serikali Na. 488 la mwaka, 2020. Tangu kuanzishwa kwake, Bodi ya Filamu Tanzania ilikuwa ikitekeleza majukumu yake kama sehemu katika Idara ya Maendeleo ya Utamaduni Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Katika jitihada za kuongeza ufanisi wa kiutendaji, kuanzia mwezi Julai, 2016, Serikali iliiwezesha Bodi ya Filamu kuwa Taasisi inayojitegemea kiutendaji ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

Baada ya Uhuru, taasisi binafsi zilijitokeza katika utengenezaji, uzalishaji, usambazaji na uoneshaji wa filamu.

Aidha, Serikali ilianzisha Taasisi na Vitengo ambavyo vilitumika kutengeneza Filamu zenye maudhui ya kuhamasisha maendeleo, umoja wa Kitaifa na matukio mengine ya Kiserikali.

Taasisi zilizoanzishwa ni pamoja na Kampuni ya Filamu Tanzania (TFC) mwaka 1968 iliyokuwa na jukumu la kupata uhalali wa kazi za Kitanzania.

Taasisi ya Vielelezo ya Dar es Salaam (AVI) mwaka 1974, Maktaba ya Filamu iliyoanzishwa mwaka 1972 na Bodi ya Filamu iliyoanzishwa mwaka 1976.

Katika kipindi hicho, Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya Mwaka 1976 ilitungwa pia. Katika kipindi cha soko huria, sehemu kubwa ya Uandaaji, Uigizaji na Usambazaji wa kazi za Filamu ulifanywa na Sekta Binafsi.

Bila kulazimika kupitia Kampuni ya Fillamu Tanzania (TFC). Baadhi ya Kampuni zilizokuwa zinashughulisha na kazi hizo ni *Pan-African Film Distributors, United Film Distributors na Anglo-American Film Distributors.*

Kuanzia miaka ya 2000, ukuaji wa Sayansi na Teknolojia umechochea kampuni binafsi za wazawa kupata mwamkio wa kuendesha Sekta za Filamu Kibiashara.

Ambapo kwa kuzalisha na kusambaza, kuonesha na kuhifadhi kazi za Filamu. Vilevile, kumekuwepo na uanzishwaji wa Vyombo vya wadau, vikiwemo Shirikisho la Filamu Tanzania na Vyama vinavyounda Shirikisho hilo pamoja na Asasi na Taasisi binafsi zinazoshughulika na uendelezaji wa Sekta ya Filamu.

Mustakabali wa Filamu Tanzania kwa miaka 59 ya Uhuru umebaki kwenye mikono ya Sekta binafsi ambazo zimekuwa zikifanya kazi zao kwa utofauti mkubwa.

Teknolojia imekua jambo lingine ambalo limeihamisha kabisa Tasnia hiyo kutoka kwenye njia ya zamani ambayo ni Tape na CD na kuhamia mtandaoni kwa maana ya YouTube pamoja na visimbuzi.

Wasanii wamebaki wachache ambao wanazalisha Filamu na kuziweka dukani. Wengi wamehamia kwenye njia ambayo nimeeleza awali. Njia ambayo kimsingi inaonekana kuwalipa Wasanii wengi.

**Dira ya Bodi ya Filamu ni:**
Kuwa na Tasnia ya Filamu shindani kwa maendeleo ya Taifa na kupunguza umasikini *(Vibrant and competitive Film industry for national development and poverty alleviation).*

**Dhima ya Bodi ya Filamu ni:**
Kuweka mazingira bora na wezeshi kwa ukuaji wa Tasnia ya Filamu. *(To create conducive and enabling environment for film industry prosperity).*

**Lengo la msingi:**
Lengo la msingi la Bodi ni Kusimamia maudhui ya Filamu pamoja na kuimarisha uwekezaji katika Sekta ya Filamu nchini.

**Majukumu ya bodi ya filamu**
Kwa mujibu wa Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya Mwaka 1976, Bodi ina majukumu makuu yafuatayo: -

(a) Kuishauri Serikali masuala yote yanayohusu Filamu na Michezo ya Kuigiza pamoja na kuratibu Sekta ya Filamu na Michezo ya Kuigiza.

(b) Kusimamia na kuratibu utayarishaji Uhakiki pamoja na kutoa vibali na kupanga madaraja ya Filamu na Michezo ya Kuigiza.

(c) Kusimamia urasimishaji wa biashara/shughuli zote zinazohusu Filamu kama vile Maktaba za Filamu, kumbi za kuoneshea Filamu/Sinema na vikundi vya Uigizaji.

(d) Kuandaa, kuratibu na kuendesha warsha, vikao, mijadala na mafunzo ya kujenga weledi kwa wadau wa Filamu, utoaji wa tuzo na uendeshaji wa Matamasha mbalimbali.

Mafanikio ya Taasisi
Bodi katika utekelezaji wa majukumu yake imekuwa na mafanikio mbalimbali. Mathalani katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi mwezi Februari, 2023 Bodi ya Filamu Tanzania imekuwa na mafanikio yafuatayo.

**Uboreshaji wa huduma na mifumo**
Katika kuondoa ombwe la upatikanaji wa huduma na kukosekana takwimu kwa wakati zinazohusu wadau wa Filamu, Bodi ya Filamu ilianzisha mfumo wa kidijiti unaojulikana kama Art Management Information System (AMIS) unaopatikana kupitia https://sanaa.go.tz,.

Ambao unatoa huduma mbalimbali na kumrahisishia mdau kupata huduma hizo bila kufika katika ofisi za Bodi ambapo hadi sasa wadau 233 wamesajiliwa na wameanza kutumia mfumo huo. Huduma hizo ni kama vile:
(a) Kujisajili na kuhifadhi taarifa za wadau, na
(b) Kutoa vibali vya Filamu, Leseni za uendeshaji wa shaghuli za Filamu, na Vitambulisho vya Bodi

**Utetezi wa Haki za Wasanii**
Katika kuhakikisha kuwa haki inapatikana kwa wasanii ikiwemo Wasanii wa Filamu, Bodi ya Filamu inaratibu Kamati ya Kutetea Haki za Wasanii iliyoundwa na Waziri mwenye dhamana ya kusimamia Sanaa nchini kwa mara ya kwanza mwaka 2018 na kuhuishwa tena 2019, 2020.

Ikiwa na mabadiliko ya baadhi ya wajumbe itakayodumu hadi mwishoni mwa mwaka 2023. Hadi sasa, kamati hiyo imeshapokea malalamiko 78 na kuyashughulikia.

Aidha, yapo malamiko 02 ambayo bado yanaendelea kushughulikiwa. Kupitia Kamati hii, zaidi ya kiasi cha milioni 316,877,447, ambacho wadau walikuwa wamedhulumiwa kimerejeshwa kwa wadau.

Baadhi ya malalamiko yaliyopokelewa na kusuluhishwa ni pamoja na yale ya:
(a) Marehemu Amri Athumani (King Majuto) ambapo familia yake ilipatiwa zaidi ya milioni 30 kama fidia ya kazi zake.

(b) Msanii wa Muziki David Ganzi (Young Dee) ambaye alilipwa kiasi cha Shilingi milioni 25 na Kampuni ya Azam Media.

(c) Marehemu Steven Kanumba ambaye mama yake alilipwa Shilingi milioni 15 na Kampuni ya Steps Entertainment.

(d) Kampuni ya Liro Productions na Twins Media walilipwa Dola za Marekani (USD) 37,000 sawa na zaidi ya Shilingi Milioni Themanini na Tano (85,000,000/=) na Kampuni ya Startimes.

Maboresho ya Sheria ili kuendana na mazingira ya sasa
Ili kuenda na wakati wa sasa katika ulimwengu wa Sanaa, Bodi ya Filamu imekuwa ikiboresha Sheria na Kanuni zake na kuondoa baadhi ya vifungu ambavyo havina mchango katika kukuza Sekta ya Flamu nchini.

Tangu kuundwa kwake mwaka 1976, Sheria hiyo ya Filamu na Michezo ya Kuigiza imefanyiwa marekebisho mara 4 (mwaka 1984, 2002, 2013 na 2019).

Aidha, Kanuni mpya za Sheria hiyo zilitungwa mwaka 2020 na kuondoa zile za mwaka 2011 lengo likiwa kuweka mazingira rafiki na kuondokana na dhana nzima ya UDHIBITI wa filamu nchini

Maboresho hayo yaliondoa baadhi ya tozo kama Ada ya uhakiki ya kila mwaka, na kupunguza nyingine kama ifuatavyo;
(a) Ada ya USAMBAZAJI kwa 92.8% (kutoka Shilingi 500,000 hadi Shilingi 36,000).
(b) Ada ya VIBALI kwa 90% kwa wazalishaji wachanga (kutoka Shilingi 500,000 hadi Shilingi 50,000), na
(c) Ada ya UHAKIKI kwa 50% (kutoka Shilingi 1,000 hadi Shilingi 500 kwa Tamthilia kwa dakika)

Aidha kwa kuzingatia mabadiliko yanayoendelea kutokea ndani na nje yaNchi hususan kwenye Tasnia ya Filamu, Bodi ya Filamu imeona umuhimu wa kuandika upya Sheria ya Filamu itakayokidhi mahitaji ya Tasnia kwa sasa na siku za usoni. Rasimu ya Sheria hiyo imeandaliwa na inaendelea kuboreshwa.

Kuimarisha miongozo ya Usimamimizi na uendelezaji wa Sekta ya Filamu
Katika kuhakikisha kuwa changamoto zinazoikabili Sekta ya Filamu nchini zinatatuliwa, mchakato wa Utungaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Filamu ulianzishwa.

Ambapo baada ya kuwasilishwa katika Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilielekezwa kuwa vipengele muhimu vilivyopo katika rasimu ya Sera hiyo vijumuishwe katika Sera ya Utamaduni ambayo kwa sasa inafanyiwa maboresho.

**Uendeshaji na Ushiriki wa Tuzo**
Ili kuhamasisha uzalishaji wa Filamu bora pamoja na kuibua na kuendeleza vipaji vilivyosheheni katika Tasnia ya Filamu nchini, bodi imeanzisha Tamasha la utoaji wa tuzo kwa wadau wa Filamu ambapo kwa mara ya kwanza tuzo hizo zilitolewa mwaka 2021 Jijini Mbeya.

Ambapo mwaka 2022 zilitolewa Jijini Arusha. Katika tuzo hizo, kulikuwa na tuzo 10 maalum zilitolewa kwa wadau/Wasanii wa Filamu (bila kushindanishwa) kutambua mchango wao katika maendeleo ya Tasnia hii.



Utayarishaji wa Filamu kipindi cha miaka ya nyuma

Ukiachilia tuzo zetu za ndani ya nchi, wadau wetu wa Filamu wameendelea kutwaa tuzo mbalimbali katika nyanda za Kimataifa. Mifano michache ni Filamu ya Vuta N'Kuvute ya Amil Shivji imeshinda tuzo 14 kwenye nchi tofauti tofauti zikiwemo Marekani, Canada, Ujerumani, Switzerland, Qatar, Burkina Faso, Rwanda, nk.

Tamthilia ya JUA KALI imeshinda tuzo kadhaa ikiwemo ile ya ZIKOMO kutoka nchini Zambia; Filamu ya BINTI JASIRI nayo imeshinda tuzo kutoka Nchi kadhaa ikiwemo Nigeria, na Filamu ya NYARA nayo imeshinda tuzo kutoka Nchi kadhaa kama vile Nigeria.

Aidha, kwa upande wa wadau mmoja mmoja, wamekuwa wakishinda tuzo kadhaa nje ya Nchi. Mifano michache ni wadau kama Christina Pande aliyeshinda tuzo nchini Rwanda, Reginah Kiwhele aliyeshinda tuzo nchini Kenya, Amil Shivji (Rwanda, USA, Quatar, German, BukinaFaso, Rwanda, na Switzalanda) Fredy Feruz (Nigeria), Seko Shamte, Leah Mwendamseke (Zambia), Joti (ZICOMO).

Masoko na Miundombinu ya Usambazaji wa Filamu
Mazingira rafiki na wezeshi yaliyowekwa katika Tasnia ya Filamu yamepelekea kuongezeka kwa fursa mbalimbali za uwekezaji kwenye miundombinu ya uzalishaji na masoko ya mazao ya filamu. Baadhi ya miundombinu iliyopo na iliyoanzishwa ni:

(a) Usambazaji kupitia vituo vya Luninga (Televisheni) katika Visimbuzi vyenye chaneli zinazoonyesha filamu za kitanzania masaa 24 siku 7 za Juma.Vituo hivyo ni pamoja na Azam Two (Azam TV), Sinema Zetu (Azam TV), Mambo TV (Star Times), Zuku, Star Swahili na Maisha Magic Bongo (DSTV);

(b) Aidha, vituo vya EATV, Clouds Plus, Azam 2, Sinema zetu na ITV navyo vina programu za uoneshaji wa Filamu za Kitanzania ama zilizotafsiriwa kwa Kiswahili kutoka lugha za kigeni (Dubbing).

Aidha Filamu ya muandaaji ya Kitanzania Bw Ernest Napolioni ijulikanayo kama Peponi imetasfsiriwa kwenye lugha ya Kifaransa na inaoneshwa kwenye televioni ya taifa.

C) Usambazaji kupitia mifumo ya kidijiti (Digital platforms) ambapo peogramu tumizi (App) zinatumika kusambaza filamu zikiwemo Swahiliflix, Vido, Netflix Kipaji App, Nilipe App, Airtel TV na Mambo TV ambazo zinatumika kuonyesha filamu za watanzania kwa makubaliano maalumu na wamiliki wa kazi hizo; na

(d) Kumbi za Sinema, ambapo kumekuwa na ongezeko la uwekezaji katika kumbi hizo. Kwa sasa Tanzania ina kumbi za Sinema za kisasa nane (8) katika mikoa ya Dar es Salaam (Kumbi 3), Arusha (Kumbi 2), Tanga (Ukumbi 1), Mwanza (Ukumbi 1) na Dodoma (Ukumbi 1);

Filamu kadhaa za kitanzania zimekidhi vigezo na kuoneshwa kwenye kumbi hizo. Hivi karibuni filamu kama Nyara, Binti, Decision, Cops Enemy; na Tamthilia za Ahadi, Turufu, Ndoano na Mwanamuziki zimezinduliwa kupitia kumbi hizo na hivyo kuendelea kuvutia wadau wengine kutumia njia hii kujiongezea mapato.



Utayarishaji wa Filamu kipindi cha miaka ya sasa

Katika kuimarisha umuhimu wa kumbi hizo kwa Watanzania, Bodi imeunda na inaratibu Kamati ya kurudisha utamaduni wa kutazama Filamu katika Kumbi za Sinema.

Uhamasishaji kwa wamiliki wa kumbi za sinema pamoja na wamiliki wa kazi za filamu unaendelea kufanyika ili kazi za filamu za kitanzania ziwe zinazinduliwa na kuoneshwa katika kumbi hizo.

Hatua hiyo inatarajiwa pia kutoa mchango stahiki katika uchumi wa wadau wa Sekta na Taifa kupitia viingilio vya mlangoni kama yafanyavyo mataifa mengine yaliyoendelea kifilamu kama Marekani, Korea Kusini, India, Nigeria, nk.

Aidha, kumekuwa na chimbuko la kumbi ndogo ndogo nyingi sana hapa nchini almaarufu Vibanda Umiza ambazo humfikia mlaji mtaani kwake. Kwa kutambua umuhimu wake katika soko/usambazaji wa Filamu nchini, Bodi imeona ni vizuri kuzirasimisha kumbi hizo na kuziwekea utaratibu ili zifanye Kazi kwa kufuata Sheria na taratibu zote. Hivi sasa Bodi iko kwenye hatua ya kuzitambua kumbi hizo nchini kote.

Kwa upande wa Kimataifa, kumekuwa na kazi za watanzania zinaonyeshwa kwenye nchi mbalimbali duniani kama vile Vuta N'Kuvute iliyozinduliwa kwenye Tamasha kubwa zaidi Duniani liitwalo Toronto International Film Festival (TIFF). Pia kwa miaka miwili mfululizo, Filamu za Kitanzania zimeonyeshwa kwenye Tamasha la Korean African Week nchini South Korea.

**Mitaji na Uwezeshaji**
Kumekuwa na ongezeko la uwekezaji kutoka sekta binafsi katika eneo la filamu nchini hasa kwenye upatikanaji wa mitaji ya uzalishaji wa kazi bora za Filamu nchini.

a. Mathalani, kwa mwaka 2021 Kampuni ya Azam Media ilitenga fedha za Kitanzania takriban Bilioni 4 (Bilioni 1 kwa ajili ya ununuzi wa filamu 1923 na Bilioni 3 kwa ajili ya ununuzi na uonyeshwaji wa zaidi ya Tamthilia 10 za Kitanzania.

Ikiwa ni ongezeko la Bilioni 1 kutoka mwaka 2020 ambapo Kampuni hiyo ya Azam Media iliwekeza zaidi fedha za Kitanzania Billion Tatu (3,000,000,000/=) katika utayarishaji na uonyeshwaji wa tamthilia za kitanzania na ununuzi wa zaidi ya filamu mia saba (700) kutoka kwa watayarishaji wa kitanzania.

b. Mfano mwingine mzuri ni Kampuni ya Multichoice Tanzania ambayo hadi kufikia mwaka 2020 ilikuwa imeshawekeza kiasi cha takriban dola za kimarekani Milioni Tatu (3,000,000 USD) kwenye uzalishaji na ununuzi wa Filamu za kitanzania.

c. Kampuni ya Star Media nayo ni mfano mwingine mzuri ambapo imeshawekeza zaidi za Milioni 280 kwenye eneo la ununuzi wa filamu za kitanzania.

**Fursa za Ajira**
Kwa upande wa ajira, Sekta hii imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika kuzalisha ajira ambapo idadi ya ajira mpya imekuwa ikikua kila mwaka.

Kwa mfano katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22 wastani wa ajira 43,680 zilizalishwa kutokana na filamu 2044 (ndefu 2009 na tamthilia 35) zilizoandaliwa hapa nchini.

Mwaka 2020/2021 filamu mpya zilizozalishwa ni 1578 (filamu ndefu 1560 na tamthiliya 18) na hivyo kuzalisha ajira takriban 33,000.

Kwa mazingira ya kitanzania Filamu moja inakadiriwa kuajiri wastani wa watu 20 ambapo tamthilia moja inaajiri wastani wa watu 100.

Kuanzishwa kwa Jarida la Bodi ya Filamu;
Katika kuhakikisha Bodi inajitangaza kupitia:
(a) Jarida lake lijulikalo kama Filmika linalotumika kuandika na kutangaza shughuli za Filamu pekee hapa nchini. Kwa mara ya kwanza Jarida hili lilichapishwa Machi 2022 na kusambazwa kwa wadau mbalimbali.

(b) Toleo la pili la Jarida hili limechapishwa na kusambazwa kwa wadau wa sanaa, taasisi na viongozi mbalimbali ambapo inatarajiwa kuwa jarida hili litakuwa kiungo muhimu cha kutoa tarifa sahihi za filamu hapa nchini.

*Youtube* TV – Bodi ina TV mtandao inayopatatikana *Youtube* (Link bodiyafilamu onlinetv1999) inayojulikana kama Bodi ya Filamu *Online TV*. Televisheni hii hutumika katika kusambaza maudhui mbalimbali yanayoandaliwa na Bodi ya Filamu Kwenda kwa wadau wake.

c. Kipindi maalum cha redio kijulikanacho kama Filmika ambacho huandaliwa na Kitengo cha Habari na Mawasiliano ni njia nyingine ya kufikisha taarifa mbalimbali za Tasnia ya Filamu kupitia redio kama vile Global radio, Midundo na Nyemo FM.

d. Mitandao ya kijamii kama vile kurasa zetu za *Facebook* na *Instagram* ambazo hufuatiliwa na zaidi ya watu 11,800 kwenye *instagram* na 4,988 kwenye *facebook* wakiwemo wasanii maarufu wa filamu kama vile Monalisa (ambaye pia ni Balozi wa Bodi ya Filamu), Isarito (mwigizaji Bora wa Kiume mwaka 2021), Celestine Gachuhi (mwigizaji maarufu kutoka Kenya aliyecheza kama Selina kwenye Tamthilia ya Selina).

Kuimarisha mahusiano kati ya Bodi na wadau wake.
Ili kuhakikisha wadau wanakuwa na mifumo imara ya uendeshaji wa Shirikisho na vyama vyao, Bodi ililiwezesha Shirikisho la Filamu Tanzania kukamilisha uhuishaji wa Katiba yake na kuwezesha kufanyika kwa Mkutano Mkuu maalum wa Shirikisho uliopelekea Shirikisho hilo kufanya Uchaguzi wa Viongozi wake pamoja na Chaguzi za viongozi wa Vyama vyake.

Vilevile, Bodi imesimamia uboreshaji wa katiba ya Shirikisho hilo kupitia Kamati Maalum/Kikosi Kazi (Task Force) iliyoundwa na Waziri ili isimamie uboreshwaji wa Katiba ya Shirikisho na Vyama vyake na Uchaguzi mwingine wa Viongozi wa Shirikisho unaotarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Vile vile, Bodi imekuwa na Vikao kikazi na viongozi wa Shishirikisho hilo kila baada ya miezi mitatu (3) kujadili changamoto zinazoikabili Sekta na kujadili kwa pamoja namna bora ya kutatua changamoto hizo.

# Mama Ni Mama

## Wanawake Nguli katika Tasnia ya filamu nchini

Miongoni mwa kazi ngumu kwa Mwanamke kwenye kutekeleza majukumu yake ya Sanaa huwa ni familia. Wote tunajua kuwa mama siyo kazi rahisi sana.

Lakini wapo Wanawake wachache ambao ni nguli na wamekuwa wakipambana kwenye Sanaa na kufanya vizuri, wakati huo huo familia nayo ikiwa inasonga katika misingi bora.
Tukizungumzia Wanawake ambao wamekuwa kioo cha jamii na watu wengi hupenda kuwatazama huwezi kuacha kumtaja Bi. Sauda Simba, Bi. Susan Lewis maarufu kama Natasha, Bi. Fatuma Makongoro maarufu kama Bi. Mwenda, Bi. Teckla Mjata, Bi.Hidaya Njaidi pamoja na Bi. Grace Mapunda.

Kwenye Makala hii tupo na Mwanamke nguli, ambaye ameanza kuonekana kwenye luninga mwanzoni mwa miaka ya 2000, akiwa kama Mtangazaji wa Kituo cha ITV.

Vijana wa wakati huo hasa wale wasomi, walikuwa wanamwangalia kuanzia saa 4:00 usiku, kwa kuwa Taarifa ya Habari yake ilikuwa ni ya kwa lugha ya Kiingereza, siyo mwingine bali ni

### BI. SAUDA SIMBA.

Mwanamke ambaye alikuwa na sura ya upole tangu akiwa binti, haiba ambayo hadi sasa kwenye utu uzima imebaki vilevile. Watoto wa mjini wanasema anazeeka na uzuri wake.

Mbali ya kuwa Sauda ni Mtangazaji, kazi ambayo aliipa kisogo kwa muda mrefu kidogo, nguvu akahamishia kwenye Biashara, Uigizaji, Ushereheshaji (MC) na mambo mengine ya familia.

Sauda kwa sasa anatamba zaidi kwenye Tamthilia ya Jua Kali akiwa kama mke wa Profesa. Leo tupo naye hapa na anazungumza kwa uchache juu ya kazi yake na changamoto za kufanya Sanaa na kuisimamia familia. Huyu hapa Kama mama umewezaje kufanya kazi ya Sanaa na majukumu ya familia kwa pamoja?

"Nina bahati kwamba bado nimeweza kuendelea na kile ninachokipenda *(My passion)* hata kwenye utu uzima.


BI. SAUDA SIMBA.

“Sina watoto wadogo kwa hivyo ni rahisi zaidi kupanga program zangu. Inabidi nipange mambo vizuri kwasababu nipo kazini pia.

“Inabidi niwe *‘Planner’* mzuri na sina muda mwingi wa kupumzika tu lakini nitapumzika nikishaanza kuchoka, bado sana (Ha ha ha).

**Ni changamoto gani umekutana nazo kama Mama katika utekelezaji wako wa majukumu ya familia na Sanaa?**
“Sina changamoto kwa kweli, labda tu ningependa saa za siku zingekuwa 48 na sio 24. Muda hautoshi kwa yote ninayotaka kufanya.

**Tukitazama wakati ule na sasa ni kwa namna gani Tasnia ya Filamu imekua ukilinganisha tulipotoka?**
“Imekua sana, fursa ni nyingi zaidi, kuna ushindani zaidi, tumeingia *Netflix* (Mimi kama mama kwenye Binti) very exciting!.

*“Series* za Jua Kali imeingia Season 6, inatazamwa Tanzania nzima na nje ya Tanzania. Inapendwa sana. Malipo Alhamdulillah si haba na milango yetu kama Wasanii na nchi inazidi kufunguka”. “Tunafanya *‘Collobrations’* na Wasanii wa Nchi nyingine, kama Ghana, South Africa na mambo ni mazuri”.

**Kama Mama umewezaje kulinda Wasifu au kwenda sambamba na nyakati zinavyokwenda?**
“Sio swala la ‘kumaintain status’, ni kuishi maisha ya kihalisia. Napenda ninachofanya, napenda kuwa-*challenged”.*

“Maisha ni mafupi na hayatabiriki. namshukuru Mola kila siku kwa maisha yangu na fursa zangu, naishi kama mimi Sauda sio kama jirani au mtu mwingine”.

“Sitamani maisha yoyote ya mtu mwingine. maisha yangu kwa kweli ni *‘Golden’ ‘ofcourse’* kuna ‘*challenges’* za kawaida za kimaisha ‘now and then but’ hakuna ‘Sunshine without rain”.

“Kwahiyo sina haja ya kwenda na nyakati nakwenda kwa nyakati zangu inatosha”.

**Sanaa imekusaidia kwa kiasi gani kukuza kipato chako au Sanaa imekusaidia kukuza kipato?**
“Haba na haba hujaza kibaba, inanisaidia kwa kweli, siwezi kuishi na Sanaa peke yake lakini inasaidia kujaza hapa na pale”.

**Sanaa sasa inalipa au tunafanya tu sababu una kipaji?**
“Inazidi kuimarika lakini nafahamu kwamba kuna wengine bado wanadhulumiwa kwenye Project zao. Kwa kweli Lamata Village inajitahidi sana kumpa thamani na heshima Msanii”.

**Kama Mama ni namna gani umehakikisha unakaa katika uhusika wako ili ujumbe uifikie Jamii?**
“Nafuata *‘Script’* na *‘Direction ya Director’* na *‘Storyline’*. Nikiwa ‘on set’ mimi sio Sauda, sio Mama, ni ile *‘character’ ninayopewa”.*

“Ninachohitaji kufanya kama Msanii ni kujitahidi kuvaa uhalisia wa hiyo *‘Character’* ili watu waniamini kwenye hiyo *‘Character’,* waone hiyo *‘Character’* sio Sauda kama Mama”.
Unawashauri nini Mabinti walioko na wanaoingia kwenye Filamu?
“Sanaa ni kazi, ni biashara, kwahiyo kufanya kazi kwa bidii, nidhamu, kufanya utofauti, *‘training and practice’* bila shaka na mtazamo *‘attitude determines altitude”.*

**Kama Mama umewezaje kulinda Wasifu au kwenda sambamba na nyakati zinavyokwenda?**
“Sio swala la ‘kumaintain status’, ni kuishi maisha ya kihalisia. Napenda ninachofanya, napenda kuwa-*challenged”.*

“Maisha ni mafupi na hayatabiriki. namshukuru Mola kila siku kwa maisha yangu na fursa zangu, naishi kama mimi Sauda sio kama jirani au mtu mwingine”.

“Sitamani maisha yoyote ya mtu mwingine. maisha yangu kwa kweli ni *‘Golden’ ‘ofcourse’* kuna ‘*challenges’* za kawaida za kimaisha ‘now and then but’ hakuna ‘Sunshine without rain”.

“Kwahiyo sina haja ya kwenda na nyakati nakwenda kwa nyakati zangu inatosha”.






**Sanaa imekusaidia kwa kiasi gani kukuza kipato chako au Sanaa imekusaidia kukuza kipato?**
“Haba na haba hujaza kibaba, inanisaidia kwa kweli, siwezi kuishi na Sanaa peke yake lakini inasaidia kujaza hapa na pale”.

**Sanaa sasa inalipa au tunafanya tu sababu una kipaji?**
“Inazidi kuimarika lakini nafahamu kwamba kuna wengine bado wanadhulumiwa kwenye Project zao. Kwa kweli Lamata Village inajitahidi sana kumpa thamani na heshima Msanii”.

**Kama Mama ni namna gani umehakikisha unakaa katika uhusika wako ili ujumbe uifikie Jamii?**
“Nafuata *‘Script’* na *‘Direction ya Director’* na *‘Storyline’*. Nikiwa ‘on set’ mimi sio Sauda, sio Mama, ni ile *‘character’ ninayopewa”.*

“Ninachohitaji kufanya kama Msanii ni kujitahidi kuvaa uhalisia wa hiyo *‘Character’* ili watu waniamini kwenye hiyo *‘Character’,* waone hiyo *‘Character’* sio Sauda kama Mama”.

Unawashauri nini Mabinti walioko na wanaoingia kwenye Filamu?
“Sanaa ni kazi, ni biashara, kwahiyo kufanya kazi kwa bidii, nidhamu, kufanya utofauti, *‘training and practice’* bila shaka na mtazamo *‘attitude determines altitude”.*




**MAMA THECLA MJATTA**

Ni Mwigizaji mkongwe wa Tanzania. Huenda mnakumbuka ile Michezo za Kuigiza kwenye redio.

Tulikuwa tunaingojea kwa hamu kila wiki, hasa kwa vile wakati huo kulikuwa hakuna Luninga miaka ya 70 na 80. Pia aliigiza katika Michezo ya Kuigiza kadhaa ya redioni.

Luninga zilivyoanza alianza kuigiza kwenye Michezo ya Luninga. Mama Thecla pia ameigiza katika Sinema kadhaa zilizowahi kutikisa miaka ya nyuma na hata sasa.

Ameigiza Filamu nyingi katika uhusika tofauti, mfano katika Sinema ya Harusi ya Mariamu aliigiza kama Shangazi yake Mariamu.

Katika Filamu ya "Maangamizi" *The Ancient One* aliigiza kama mama wa Mhusika Mkuu, Samehe. Samehe, alishuhudia kifo cha kuunguzwa na moto na baba yake mzazi ambaye alikuwa ni Mchungaji mwenye imani kali ya Dini.

Sinema ya Maangamizi ilichaguliwa kama sinema ya kwanza kutoka Tanzania, katika Tuzo za Akademi 2001 kwenye kipengele cha *'Foreign Language category'.*

Pia ameigiza katika Filamu ya Simu ya Kifo, Tumaini, Mzee Mkude, na Mlima Kolero. Kisha akapita kwenye Filamu ya Bongoland II, akicheza kama mama yake Mhusika Mkuu, Juma.

Huyo ni Mama Tecla wa zamani, lakini huyu wa sasa anatisha sana kwenye Tamthilia zinazoruka Azam TV, DSTV na kwenye Luninga nyingine nyingi na kwa sasa anatamba na Tamthilia ya "Fungu Langu" inayoruka Azam TV.

Makala hii inazungumza na mama huyu ambaye ameweza kudumu kwa miaka mingi sana kwenye Tasnia ya Filamu na Tamthilia na tumezungumzia machache kuhusu kazi yake.

**Ni kwa kiasi gani unafurahia kazi yako ya Sanaa?**
"Sanaa ni kazi kama kazi zingine kwahiyo niliweza kupangilia ratiba ambayo imeniwezesha kutimiza majukumu yangu bila shida na familia yangu inaielewa na kunisaidia".

**Changamoto unazokutana nazo kwenye kazi yako ya Sanaa ni zipi?**
"Changamoto nilizokua nazo ni pale mmoja wa familia ana shida yoyote inayotaka nimuhudumie na mimi natakiwa kazini".
"Kazi yangu nafanya kama mlolongo, hivyo ikitokea wewe haupo ina maana wenzako nao watasimama au labda atafutwe mbadala". **Ni mafanikio gani umeyapata kwenye Sanaa?**
"Sanaa sasa inalipa, nimefanya Sanaa kwa kuwakilisha kipaji changu na kupata kipato.

**Una ushauri gani kwa Mabinti chipukizi kwenye Tasnia?**
"Mabinti wanaongia kwenye Sanaa nawashauri wazingatie Sheria za Nchi yetu, wazingatie mila na desturi zetu za Kitanzania.

"Watangaze na kukuza Kiswahili kama lugha ya Taifa, watumie Mitandao kwa usahihi wawe wavumilivu na ustahimilivu, wapende vya kwao na Elimu haina mwisho.

**BI MWENDA**




Uchawi wake kwenye Filamu umempa nyumba MOJA kati ya Waigizaji ambao pengine hadi sasa wanachukuliwa kama watu wabaya kwenye jamii kutokana na maigizo yao basi ni Bi Mwenda, ambaye amezoa umaarufu wa kucheza kama mchawi na Mama mkali na mwenye roho mbaya.

Alianza kutikisa kwenye Filamu na Tamthilia tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000. Wengi wanamjua huyu Mama kwa kazi tu na hawajui Historia yake. Sasa Makala hii inakupa mambo mengi usiyoyajua kuhusu Bi Mwenda.

**Historia yake**
Bi. Mwenda ni mzaliwa wa Mara Wilaya ya Bunda Kijiji cha Ikwizu Nyamuswa, ni mtoto wa Mtemi Makongoro, ambaye alikuwa rafiki na ndugu wa yamini na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Anasema katika maisha yake wakati yupo darasa la tano mpaka anamaliza alikuwa akiishi Kinondoni karibu na Mahakama ya Kinondoni. Wakati huo wenzake walikuwa wakisoma Shule ya Mwenge na kupelekwa na gari.

Bi Mwenda, anasema alijiingiza kwenye michezo mbalimbali akiwa darasa la nne. Katika Shule ya Msingi Ikwizu alijihusisha na michezo mbalimbali kama Ngoma za asili, Netiboli na Mbio za kijiti.

"Mara nyingi nilikuwa nikijitolea, kwa kuwa michezo ilikuwa ndani ya damu," anasema Bi Mwenda. Anasema alipomaliza Elimu ya Msingi, kwa kuwa alikuwa hana kazi nyingine ya kufanya ndipo akaolewa, akiwa ndani ya ndoa alikuwa hajihusishi na jambo lolote zaidi ya kukaa nyumbani kama Mama wa familia.

Hata hivyo anasema mwaka 1998 ndipo alipotamani tena kurudi kwenye Michezo ya Kuigiza hasa na zaidi alivutiwa na Uigizaji.

Anasema watu ambao kwa kipindi hicho walimvutia sana katika kuigiza alikuwa Mzee Onyango, Mzee Bashir na Mwita Maranya waliokuwa wakiunda kundi la Tausi na Wasanii Waridi, Richirich, Bishanga ambao walikuwa wakiunda kundi la Mambo Hayo.

Anasema alitamani sana kuigiza kwa kuwa uigizaji upo ndani ya damu yake na kuongeza kuwa muda huo ndipo akakutana na Kiongozi wa kundi jipya la Kaole Sanaa Group na hatimaye kujiunga na kundi hilo.

"Kipindi hicho kundi la Kaole lilikuwa na watu 14, ambao ndiyo walionipokea," anasema huku akifikiria majina ya watu hao. Bi Mwenda anasema miongoni mwa Wasanii aliowakuta hapo ni Mzee Pwagu, Mzee Kipara, Mama Haambiliki na wengine, wakiwa chini yaUuongozi wa Chriss Muhenga.

Kwa mara ya kwanza kundi hilo lilianza kuandaa filamu kwa mfumo wa mkanda na Filamu hiyo ilijulikana kwa jina la 'Ndoa ya lazima'. Hata hivyo, hawakufanikiwa kuutoa mkanda huo.

"Kwa sababu walipata nafasi ya kupeleka mchezo wao katika kituo cha Televisheni cha ITV baada ya kikundi kilichokuwepo kuondolewa.

Mchezo wao wa kwanza kurushwa uliitwa 'Kabla Hujafa Hujaumbika' ambao Bi Mwenda aliigiza kama Mama yake Dk. Cheni. Igizo hilo lilimpatia umaarufu mkubwa, hasa alipoigiza kama Mama Mchawi, akishirikiana na Muigizaji mwenzake mfupi Mlopelo kuwaloga watu na kuwageuza paka.
Anasema kwenye igizo hilo aliweza kuuva uhusika, ambao ulimpelekea kila mmoja kuwa na mawazo tofauti juu ya uhalisi na uigizaji wake wa uchawi.

"Sikuwa na lengo lolote zaidi ya kuelimisha jamii kwamba matukio kama hayo yapo. Lakini Waandishi na jamii ikaanza kunijadili tofauti,"anasema.

Tangu hapo Bi Mwenda anasema akaanza kupata mialiko ya Filamu za nje, wakitaka aigize uhusika wa Mama mchawi au mwenye roho mbaya, sababu aliweza kuuvaa uhusika huo vizuri.
Anasema yeye hakuweza kukataa kwa kuwa alikuwa akiongozwa na Muongozaji wa Filamu pamoja na mswada wa filamu (Script) yake inavyosema.

Akiwa kwenye Kundi hilo alishiriki katika maigizo mbalimbali ikiwemo, 'Hujafa Hujaumbika', 'Fukuto', 'Jahazi', 'Dira', 'Tetemo', 'Tufani', 'Sayari', 'Baragumu', 'Gharika', 'Taswira' na 'Zizimo.

Kundi hilo pia lilikuwa na Wasanii mbalimbali wakiwemo Steven Kanumba, Vicent Kigosi 'Ray', Muhogo Mchungu, Kipemba, Dk. Cheni, Mtunisi, Frank, Nina, Nana, Norah, Sinta, Kibakuli, Nyamayao, 'Max', Zembwela, na Bambo.
Wengine ni Kingwendu, Kemmy, Benny, Swebe, Chuz, Mashaka, Kissa, Johari, Mainda, Thea, Maya, Sajuki, Dino, Pembe, Senga, Tito, Mboto, Kelvin, Zawadi, Bi Kidude na wengine wengi.

Bi. Mwenda anasema katika Uigizaji wake hatoweza kusahau matukio mengi yaliyomkuta ambayo yalimkatisha tamaa na kutaka kuachana na Uigizaji.

Anasema hii inatokana na kuuvaa uhusika na wapo wengine ambao wana matendo kama hayo, hivyo wanahisi kama wanadhalilishwa na kufichuliwa kwa kazi zao na ndiyo maana walikuwa wakimwandama.
Hali ambayo anasema ilichangiwa sana na baadhi ya Vyombo vya Habari vilivyokuwa vikimwandika bila ya uchunguzi na jamii ikawa ikimwangalia vibaya.

Kwa mujibu wa mama huyu miongoni mwa matukio ambayo hatoyasahau ni la mwaka 2002, akiwa katika maeneo ya Kariakoo sokoni alipokwenda kununua mahitaji.

Mwaka 2005 ndipo Bi Mwenda akajiingiza kwenye Uigizaji wa Filamu, na alianza kwa kushiriki filamu iliyokuwa ikijulikana kama Riziki, iliyoandaliwa na Chiki Nchome akiwa kama Mama yake Steven Kanumba.
Aliendelea kuigiza filamu mbalimbali ambazo zipo zilizofanikiwa kutoka kama vile Johari na nyingine.

Anasema hadi sasa hamna maslahi makubwa kwenye Filamu kwa kuwa bado wananyonywa na Wasambazaji kutokana na usimamizi mbovu wa Serikali.

Bi, Mwenda anasema fedha kidogo wanazopata hutumika kwa ajili ya kujikimu katika maisha ya kila siku.
Anaishauri Serikali kuwaangalia na kuwajali Wasanii Wakongwe, hasa kutokana na wao kujitolea katika kuchangia majanga makubwa na kutoa mfano namna Wasanii walivyosaidia waathirika wa mabomu Gongo la Mboto, mafuriko na mengine.

Bi Mwenda anaiomba Serikali kutambua mchango wao na Wasanii wanapozeeka waweze kuwekewa fungu kwenye Wizara ya Michezo na Utamaduni. Fedha ambazo zitakuja kuwasaidia kipindi ambacho wanakutwa na matatizo kama yalivyotokea kwa marehemu Saidi Fundi 'Mzee Kipara'.

**Kama Mama umewezaje kufanya kazi ya Sanaa na Majukumu ya Familia kwa Pamoja?**
"Majukumu ya Sanaa yanakua pembeni na majukumu ya nyumbani hivyo, nikiwa nyumbani majukumua yananisubiri, ni kuweza kubalansi".

**Ni changamoto gani umekutana nazo kama Mama katika utekelezaji wako wa Majukumu ya Familia na Sanaa?**
"Changamoto zipo za kawaida, lakini kubwa ilikuwa familia yangu ilikua haipendi nifanye kazi yangu. Nikakomaa, baadae wakakubali na wakaipenda".

Tukitazama wakati ule na Sasa ni kwa namna gani Tasnia ya Filamu imekua ukilinganisha tulipotoka?
"Tulipotoka palikuwa pagumu sana, tulikuwa tunafanya kazi tukiwa hatuna kitu mfukononi. Lakini kwa sasa utandawazi umekua na angalau tunapata kitu kwa sasa".

**Kama Mama umewezaje kumaintain status au kwenda Sambamba na nyakati zinavyokwenda?**
"Kiukweli ni utundu tu wa mambo ya kisasa kama simu na kuona namna ambavyo mambo yanavyokwenda na hiyo imefanya nisipate shida yoyote".

**Sanaa imekusaidia kwa kiasi gani kukuza kipato chako au sanaa imekusaidia kukuza kipato?**
"Binafsi Sanaa yangu imenisaidia kupata vitu vingi sana, kujuana na watu, kusomesha watoto wangu ambao walikuwa yatima, nina kibanda changu kwa sasa. Mambo yanaenda namshukuru Mungu".

**Kama Mama ni namna gani umehakikisha unakaa katika uhusika wako ili ujumbe uifikie Jamii?**
"Mara nyingi huwa nategemea zaidi muongozaji wa stori na ujumbe kwa kweli unafika na ndiyo maana watu wanapenda kazi zetu".

**Sanaa sasa inalipa au tunafanya tu sababu una kipaji?**
"Kwa sasa uongo mbaya tunapata kitu tofauti na zamani ambapo tulikuwa tunaigiza kwa sababu tunapenda na tuna vipaji".

**Unawashauri nini mabinti walioko na wanaoingia kwenye filamu?**
"Wathamini na wakipende kitu ambacho wanakifanya na waone hii ni kazi kama kazi zingine



# MIAKA 24 YA HIDAYA NJAIDI NDANI YA BONGO MUVI



KATI ya Wanawake 10 Wakongwe wanaoendeleza Tasnia ya Filamu nchini Tanzania huwezi kuacha kumtaja Mama Hidaya Njaidi.

Anasema alianza kazi za Filamu mnamo mwaka 1999 ambapo kazi zao zilikua zikirushwa kwenye Televisheni ya Ctn na Dtv kama wadau wa kazi za Sanaa.

Hidaya Njaidi ni Mama wa Watoto 5 ambapo watoto 4 wamefuata nyayo zake za kazi za Filamu na kutambulika vizuri kwenye Kiwanda cha Bongo Muvi akiwemo Othman Njaidi maarufu kama Patrick Kanumba.

Pia anaeleza kuwa Kipaji cha Mtoto wake Patrick Kanumba kiligunduliwa na Marehemu Director Kombo tangu Patrick akiwa na miaka miwili huku Filamu yake ya kwanza kucheza akiwa na miaka 9 iliyoitwa “White Maria”.
Ameongeza kuwa anajisikia fahari sana kuona nyumba hiyo iliyojaa vipaji inafanya vizuri ndani na nje Kimataifa ambapo Patrick ameanza kuonekana kwenye Filamu Afrika Mashariki.

Aidha, Njaidi alishiriki tamthilia ya “Hukumu ya Tunu” ambayo ilimtambulisha vyema ambayo iliruka mubashara ITV ikisheheni waigizaji mbalimbali akiwemo Tecla Mjata, Seif Mbembe, Hashim Kambi na Richard Mshanga “Masinde”.
Aidha kuja kwa Wadau mbalimbali akiwataja Azam TV kuwapa nafasi kubwa Wasanii pamoja na Waandaaji wa kazi za Sanaa kupata nafasi ya kuonesha ujuzi wao.

Hata hivyo Hidaya Njaidi tayari ameshafanya Tamthilia ya “Panguso”, “Hatia”, “Turufu” pamoja na “Fungu Langu” akiendelea kubeba uhusika wake kama Mama huku akishiriki kwenye filamu nyingi.
Pia amesema kwa mwaka 2023 amejiandaa kuachia Project kutoka katika Kundi lake la Umoja wa Wanawake Wajasiriamali Tanzania (UWAWATA).

Ambapo kundi hilo ni mkusanyiko wa Wasanii mbalimbali akiwemo Cathy Rupia, Jennifer Kyaka pamoja na Ndumbangwe Misayo (Thea).

Hata hivyo amewapa habari njema wadau wa Filamu kuwa amechaguliwa kuwa Muongozaji Mkuu wa kuandaa Tuzo za Filamu Afrika Mashariki kwa Filamu zinazotumia Lugha ya Kiswahili.



# MATUKIO NA PICHA



Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Dkt. Kiagho Kilonzo pamoja na Yvonne Cherrie (Monalisa) wakiwakaribisha Jacqueline Wolper, Salim Ahmed Issa (Gabo Zigamba) katika makubaliano ya kuwa Balozi wa Bodi ya Filamu.



mapokezi ya Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo Mhe. Pindi Chana katika ofisi za Bodi ya Filamu.



Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania Dkt. Kiagho Kilonzo ambaye pia ni mlezi wa Tuzo za Wanafunzi wa Vyuoni wenye vipaji mbalimbali “UNIAWARDS” akikabidhi Tuzo ya Muandaaji Bora wa Filamu Bw. Godwin Lukio.




Moja ya wadau wa Filamu waliopewa mkopo kwa nia ya kukuza na kuboresha kazi zao.




OSCARS TZ COMMITEE - Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya kuchagua Filamu kutoka Tanzania itakayoshiriki Tuzo za Oscars.

# SEKO SHAMTE

**Mwanamke Mtanzania wa kwanza aliyeitikisa Dunia Netflix**




**Seko Shamte akiwa pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan katika picha ya pamoja.**

Seko Shamte, hili siyo jina geni kwenye Tasnia ya Filamu Tanzania, Afrika na dunia kwa jumla mara baada ya kazi yake ya Binti kuweza kufika Netflix na kuwa Filamu ya kwanza kuweka rekodi hiyo.

Binti ni Filamu ambayo iliweza kushika nafasi ya tatu kwenye Netflix duniani na rekodi hiyo iliwekwa hadharani na Forbes ambao walifikia hatua ya kuitangaza ulimwenguni kuwa ni Filamu kali ya kuitazama.

Seko, ni Muongozaji wa Filamu na Mtunzi wa hadithi mbalimbali, amekuwa ni Mwanamama ambaye anatengeza Filamu nyingi fupi kama vile “Sweta”, “Mid Night”, “Jikoni”, “Home Coming” na nyingine.

Seko Shamte alikulia Dar es Salaam lakini alitumia baadhi ya miaka yake ya utotoni kuishi huko Marekani na Asia.

Wazazi wake, Fulgence na Antonia Tingitana, Baba Mhandisi (Injinia) na mama, Mtaalamu wa Elimu alihimiza ukuzaji wa ustadi wake wa Uandishi kwa kumpeleka kwenye kambi za Uandishi wakati wa likizo za Kiangazi.

Katika Shule ya Sekondari ya Mzizima alikosoma alianza kuthamini historia na Muziki. Alicheza fidla (Violin) na alikuwa Mwenyekiti wa klabu ya muziki.

Kipaji chake kiliwavutia watu wengi sana na wakati wa mashindano ya Sanaa pale Shule ya Zanaki Sekondari, alikuwa Mwanafunzi aliyetembelea Radio One ambao walirekodi uimbaji wake uliosikika kwenye Kituo hicho.

Hiyo ikamfanya kuwa maarufu na kufahamika zaidi kwa kazi yake akiwa na miaka 17 tu. Uigizaji huo uliendelea kumpa nafasi ya kuingia katika Tasnia ya Habari na Kipindi chake katika East Africa Radio.

Maisha yake Binafsi
Ni Mke halali wa Rapa wa zamani wa Bongo Fleva Amour Shamte aliyefanya kazi miaka ya 90 na Marapa Wakongwe kama Balozi. Amour ni Mtaalamu wa masoko na Mitandao.

Ambapo Seko mwenyewe anasema, Amour ni mtu ambaye anaelewa sana mambo ya Filamu na amekuwa akimsapoti sana kwenye kazi zake tangu anaanza, Lakini pia amekuwa akimkosoa pale anapofanya vibaya na kumsifia pale anapofanya vizuri na wakati wote amekuwa akimtia moyo kuwa atatoboa kwenye kile ambacho anakifanya.




**Seko Shamte akifurahia mafanikio yake kwa kupokea tuzo ya** *“ Women In Management Africa”*

## Kazi zake alizofanya

Baada ya kumaliza Elimu yake katika masuala ya fedha na Masomo ya Vyombo vya Habari katika Chuo cha Marymount Manahattan College na mwaka wa 2005 akaenda kufanya kazi katika East Africa Television kama Mkuu wa Utayarishaji wa Vipindi.

Akiwa katika kituo cha Televisheni aliona Uandaaji na Utangazaji wa Vipindi vya Televisheni maarufu vya Ze Comedy, Friday Night Live, 5 Live! na Nirvana.

Aanzisha kampuni yake
Seko Shamte alianzisha Kampuni yake ya Uandaaji, Alkemist Media mwaka wa 2008 na kutengeneza vipindi na filamu kuhusu Tanzania na Afrika kwa ajili ya kusambazwa kimataifa.

Akianza na kazi ya kushirikishwa kwenye kazi ya Inside Africa za CNN, ikiwa ni pamoja na hadithi ya Hashim Thabeet, Mchezaji wa mpira wa Kikapu wa NBA wa Tanzania na mchango wake kwa jamii yake ya Watanzania.

Hadithi juu ya uhamiaji wa wanaume wa Kimasai nchini Tanzania (Inside Story). Hii ilifuatiwa na mfululizo wa vipande vingine vya CNN, Mitandao ya ABC nchini Marekani na BBC nchini Uingereza.

### Filamu zilizomtoa

Seko anasema, mnamo 2011, alifanya Filamu yake ya kwanza yenye urefu wa Filamu za kawaida, "Mkwawa": Shujaa wa Mashujaa. Filamu hii alikuwa ameiandaa kwa miaka 16, ukosoaji wa Mwalimu wa historia kuhusu Chifu Mkwawa kuwa 'Mwoga, kama Viongozi wengi wa Kiafrika walivyo, hiyo ilikuwa dhamira yake kubwa.

Anasema Mkwawa ulimpa utulivu na kutaka kupinga ukosoaji huo, alijifanyia utafiti historia ya Chifu Mkwawa. Hadithi ilipokuwa tayari, aliomba Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF) na kushinda ruzuku hiyo.

### The Team Tanzania

Kufuatia Mkwawa kufanya vizuri, alikwenda kuandika, kutengeneza na kuongoza mfululizo wa Filamu ya *"The Team":* Tanzania.

Hadithi hii iliangazia ukosefu wa usawa wa kijinsia nchini Tanzania ikilenga kubadilisha Kanuni za kijinsia za jamii.

Hadithi hii ina Wasichana wawili matineja, Upendo na Sophia, na mapambano yao ya kutafuta utambulisho.

Mfululizo wa sehemu kumi na tatu ulishirikiana na NGO ya Search for Common Ground na kurushwa hewani na East Africa Television.


Mfululizo huo umeendelea kutazamwa kwenye jukwaa la YouTube.

### Home Coming

Mwaka 2015, Filamu yake ya" Home Coming" ilitolewa jijini Dar es Salaam. Hadithi hii ni uchunguzi juu ya ufisadi na jinsi inavyoendelea yenyewe, kizazi baada ya kizazi.

"Home Coming" ilipokelewa vyema na Tasnia ya Filamu Tanzania. Filamu iliendelea kuchaguliwa kucheza katika Tamasha la Filamu la Pan African mwaka wa 2017.

Kisha akaandaa kazi zingine kama "Jikoni" na "Marion" iliyokuwa inaruka DSTV mwaka 2015, "Mid Night ya 2018", "Sweta" ya mwaka 2023 ambayo imechezwa pakubwa na Mpoki na Riyama Ally na kisha akatikisa Dunia na Binti.




### Binti ilikujaje?

"Baada ya kufanya kazi kwa muda mrefu kwa mwendelezo uleule bila kuvunjika moyo ndiyo nikapata nafasi ya kufanya Binti, ambayo nilianza kuifanya mwaka 2018 na ikapata nafasi 2021 takribani miaka miwili".

"Hii haikuwa labda nilikuwa na mtu Netflix bali ni kwa kuwa nilikuwa nafanya kazi kwa bidii na hatimaye nimefanikiwa kufikia hapa ambapo nimefika na nashukuru Binti imenifungulia Dunia".

Binti inahusu nini?
"Binti inahusu Wasichana wanne Wapambanaji, Tumaini ambaye alikuwa anapambana na biashara ndogondogo ili aweze kutoboa, mwingine ni Angel, huyu amefanikiwa kidogo ana biashara yake ya kuuza nguo za harusi.

"Lakini shida yake ni kwamba ana matatizo ya kimaelewano ya kimahusiano, kuna Stellah, huyu yeye ana Mume wake na wanapendana sana, lakini anakosa amani na ndoa yake kwa kuwa hawana mtoto, wa mwisho ni Rose, huyu ni mama lakini kuna mtoto wake anamuhitaji zaidi.

"Kwahiyo inaonesha ni jinsi gani Wanawake hawa wanapambana kwa namna tofauti kutatua changamoto zao".

Ushauri wake kwa Waongozaji wa Filamu
"Kikubwa ni kujifunza na kufanya kazi kila siku, kwa kuwa huwezi kufanikiwa kwa siku moja, lazima ufanye mara kwa mara bila kuvunjika moyo.

"Usiwe na haraka, usifikiri kuwa mafanikio yanakuja kwa haraka na usitamani mafanikio ya mtu mwingine, mtu asimamie anachokiamini".

"Kitu cha mwisho ni nidhamu tu, fanya kila kitu kwa kuamini kuwa kitafika mbali'.




Uzinduzi wa Filamu Tatu za Sweta, Jasiri na Nia zenye maudhui ya kutoa elimu ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi. Filamu hizi zimeandaliwa na Muandaaji na Muongozaji wa Filamu Nchini Bi. Seko Shamte.

# HASARA ZA KUSOMA

## VYUO VIKUU NJE YA NCHI

*Imeandikwa na **Aloyce Mkwizu***

Kwa miaka mitano sasa, nimesaidia wanafunzi zaidi ya elfu moja kupata nafasi katika vyuo vikuu nje ya nchi, India, Uturuki, Cyprus, Marekani, Spain, Dubai, Canada, Ujerumani nk

Wengi tunajua faida za kusoma vyuo vikuu nje ya nchi ambazo ni pamoja na elimu bora, kukutana na watu, mazingira na tamaduni mbalimbali, kujifunza lugha mpya na uwezekano wa kuanzisha maisha huko baada ya kusoma.

Licha ya faida zote hizo na nyingine nyingi ambazo sio dhumuni ya andiko hili, leo nitaongelea hasara zinazotakana na kusoma vyuo vikuu nje.

**1. Hatari ya ushoga**

Kama mwanafunzi hajajiandaa vizuri kisaikolojia au kufunzwa vizuri kabla ya safari, anaweza kukutana na *peer pressure* kubwa sana hasa katika nchi za ulaya ambapo ushoga umekithiri sana hivyo kushawishika kujiunga na vitendo hivyo. Nchi kama India, China na Falme za kiarabu, Dubai hatari hii ni ndogo sana kwani ushoga haujashamiri sana.

**2. Gharama kubwa**

Kama hujapata *scholarship,* ni vyema kujipanga vizuri kifedha kwani gharama za kusoma vyuo vikuu nje ya nchi zinaweza kuwa kubwa. Kuna hidden costs kama bima afya, gharama mbalimbali za maisha kama vile chakula, usafiri zinaweza kubwa sana hasa katika nchi za ulaya, marekani na canada. Nchi za Asia kama vile India, China, Uturuki na Cyprus gharama za maisha ni ndogo sana ndio maana huwa nashauri kama bajeti ni ya kawaida ni vyema digrii ya kwanza mtu akasome India au China

**3. Hatari ya madawa**

Asilimia ndogo ya vijana wanaohitaji ungalizi wa karibu huwa wanajisahau wanapoenda kusoma vyuo vikuu nje ya nchi na kujiingiza kwenye makundi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, *cocaine na heroine* ambazo pia ni very addictive hivyo kupelekea kumpoteza mwanafunzi kiafya na kiakili pia kwani itamfanya asahau lengo lilompeleka nje ya nchi.

**4. Kutapeliwa**

Wanafunzi na wazazi wengi wamekuwa wakitapeliwa katika safari zao kuelekea vyuo vikuu nje ya nchi, either kwa kupewa vyuo ambavyo havitambuliki nchini au kudanganywa gharama za ada za vyuo husika na maagent au watu wanaowasaidia kufanya *application.*

Wanafunzi wengi pia wanachagua *kuapply online* kwa kukwepa gharama za *service fee* bila kujua utapeli wa mtandaoni umeshika kasi sana katika karne hii 21.

**5. Hatari za kiafya na uhai**

Hi hasara mara nyingi huwa ni ya bahati mbaya lakini ni vyema kujitahadhari na maeneo au nchi ambazo hazina usalama kama vile Ukraine, Iraq, Iran Afghanistan, Sudan na Russia

Licha ya hasara tajwa hapo juu, kusoma vyuo vikuu nje ya nchi kuna faida nyingi sana na hiyo imeonekana tayari kwa walioenda wakahitimu na kurudi nchini. Kama unahitaji kusoma vyuo vikuu nje ya nchi, karibu ofisini kwetu floor ya **5, Tanzanite Park, Victoria, Dar es salaam au piga simu 0747173931 tutakusaidia.**
**#studyabroad #vyuovikuunje ya nchi**


tassaa99
0767 249 001
0785 200 313
0789 961 223

TASSAA

SASA NI RAHISI KUPATA CHUO NJE YA NCHI KUPITIA TASSAA STUDY ABROAD

5, TANZANITE PARK, VICTORIA





tassaa99
0767 249 001
0785 200 313
0789 961 223

Study MBA Online with TASSAA
Study in Canada with TASSAA
Study in Dubai with TASSAA
Study in USA with TASSAA
Study in Poland with TASSAA
Study Medicine abroad with TASSAA

Bajeti ya million 7 tu kwa mwaka inatosha kulipa Ada, malazi na chakula vyuo vikuu nje ya nchi.
Tutafute TASSAA, +255 (0) 747 173 931 tutakusaidia kutimiza ndoto zako

BODI YA FILAMU TANZANIA INACHAPISHA JARIDA LAKE LA FILMIKA LITAKATOLEWA KILA BAADA YA MIEZI MIWILI.

Kuna fursa ya kutangaza huduma au bidhaa zako kupitia jarida hili kwenye kipimo (size) cha A4 litakalosambazwa kote nchini

Robo Kurasa 300,000/=
Nusu Kurasa 500,000/=
Kurasa nzima kawaida 950,000/=
Kurasa ya nyuma 3,000,000/=
Kurasa nzima maalum 1,500,000/=
Kurasa ya ndani ya jalada la mbele 2,000,000/=
Kurasa namba 3 2,500,000/=
Kurasa ya ndani ya jalada la nyuma 2,000,000/=

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI: +255 (0) 625 320238

# MJUE MSANII WAKO

## IDRIS SULTAN





KWENYE majina ya Mastaa ambao wanafanya vizuri kwa sasa Bongo ambao wanapiga miguu yote, basi kwenye majina 10, lazima litakuwepo la Idris Sultan.

Mwamba amekuwa akifanya vitu vingi sana ambavyo vinahusiana na Sanaa hasa hii ya Maigizo na Tamthilia. Idris amekuwa akifanya Sanaa yake kwa njia tofauti sana ambayo ni watu wachache sana ambao wanaweza wakafanya kama anavyofanya.

Utamkuta kwenye Vichekesho, Utani, Maigizo, Tamthilia na hata baadhi ya matukio ya mtandaoni. Yaani ukiingia kwenye ukurasa wake wa Instagram unaweza ukaelewa hiki ambacho nakuambia.

Jina la Idris lilishika masikio ya watu wengi Afrika Mashariki na Kati na Afrika kwa ujumla, baada ya kufanikiwa kuwa Mshindi wa Big Brother Africa. Hapo akapiga mpunga akarudi zake Bongo.

Umaarufu wake ukaongezeka maradufu mara baada ya kutoka kimapenzi na Wema Sepetu, tena Wema yule wa moto ambaye alikuwa akikimbiza mitaa mbalimbali ya mjini.

Kisha akajikita pia kwenye Utangazaji wa radio, mara baada ya kupata mchongo wa kuwa Mtangazaji wa Choice FM. Ambako alikutana na watu kama Gigy Money kama Mfanyakazi mwenza.

Jamaa alikutana na kitu kizito, kwani kwa mujibu wake yeye mwenyewe, ule mpunga aliopata Big Brother Africa ambao ni takribani milioni 400 za Bongo ulikwenda na maji.



Matumizi pekee aliyofanya kwa mujibu wake ni kununua ndinga yenye thamani ya milioni 50. Huku mpunga mwingine ukipotea kimaajabu wakati anafanya michakato mingine.

Mwamba akapitia msoto kiasi cha kukosa sehemu ya kuishi, Mshikaji wake Dokta Ulimwengu ndiye aliyekuwa naye kwenye msoto huo, hadi pale walipofanikiwa kupata mchongo wa Ubalozi kwenye Kampuni moja ya kubashiri.

Baada ya mapambano mengi, jamaa akajipanga na kufikia mafanikio ambayo ameyakalia sasa hivi, akiwa na michongo ya Ubalozi na Makampuni makubwa.

Huku kwenye upande wa Filamu na Tamthilia akiwa amefika hadi *Netflix* huko, jambo ambalo siyo la kawaida na rahisi kulipata. Idris ana mambo mengi sana  anafanya ambayo wengi hawajui.

Makala hii, imempata Idris ambaye anazungumza kwa uchache juu ya kazi zake na maisha yake ya Sanaa kwa ujumla wake. Hapa anaanza kutujuza kuhusu historia yake.

**Idris ni nani?**
"Idris Sultan alizaliwa Januari 28, 1993 ni Mwigizaji, Mchekeshaji na Mtangazaji wa radio ambaye alishinda *Big Brother Africa 2014*. "Ni kijana machachari mwenye juhudi nyingi na maarifa aliyepata umaarufu kupitia Filamu ya Kiumeni (2017).

"Anajulikana nchini Tanzania kupitia Machapisho yake ya Vichekesho kwenye kurasa zake za kama *YouTube, Instagram* na majukwaa mengine.

"Tamthilia mbalimbali nilizowahi kutayarisha ni pamoja na "Ndomu" iliyokuwa inaruka, "Nakupenda Kufa" ambazo zilikuwa zinaruka *YouTube* tu".

"Tamthilia ya "Danga" ilikuwa inaruka *YouTube* na DSTV na Tamthilia niliyowahi kushiriki ni Ahadi ilikuwa inaruka Azam TV".

"Filamu nilizoweza kuandika na kuigiza ni pamoja na *"Married to Work"* (2023), ambayo inaonyeshwa *Netflix*, "Kiumeni" (2017) ambayo ilioneshwa Cinemax na *"Slay"* (2021) iliyooneshwa *"Netflix"*.

Kwa upande wako Sanaa ina msaada gani?
"Ni swali pana kujibu kwa jibu moja, ila kwa ufupi na urahisi nitajibu kwenye pande mbili, msaada wa Sanaa kwa msanii 'individual', lakini pia kwa Taifa kwa ujumla wake.Kama msanii, Sanaa inafungua milango ambayo mwanzoni ilikua imejifunga, kuanzia kunitambulisha kwenye jamii, jambo ambalo kibiashara linanirahisishia mambo mengi sana. Kitaifa, Sanaa inanipa nguvu na nafasi ya kuiwakilisha Tanzania nje ya mipaka na kuunganisha tasnia ili kujenga daraja kwa tasnia yetu kukua zaidi".

**Nje ya Uigizaji unajishughulisha na nini kingine kwenye Tasnia ya Filamu?**
"Nje ya Uigizaji mimi pia ni Mwandishi, Mtayarishaji na Mwongozaji wa Filamu.

**Mafanikio yako katika Sekta ya Filamu?**

"Sanaa imenipa vitu vingi lakini kikubwa zaidi ni kufahamiana na watu ndio kunanisaidia kuwa Idris ambae mnamuona hivi sasa yupo kwenye majukwaa makubwa kubwa, kwaajili  ya hiyo Network naweza kusema.

# TUZO
# ZA FILAMU 2022

**Washindi, Matarajio na  Mwendelezo wa Tuzo hizo.**



KATIBU MTENDAJI WA BODI YA FILAMU DKT. KIAGHO KILONZO AKIKABIDHI TUZO KWA MSANII BORA WA KIKE CHAGUO LA WATAZAMAJI **WANSWEKULA ZACHARIA**

KAMATI ya Tuzo za Filamu walitaja rasmi Vipengele 32 pamoja na Washiriki 162 waliaowania tuzo hizo zilizotolewa Disemba 17, 2022 Jijini Arusha.

Akizungumza na Wandishi wa Habari na wadau wa Filamu Disemba 9,2022 Jijini Dar es salaam Mkurugenzi wa Maendeleo ya Filamu kutoka Bodi ya Filamu Emmanuel Ndumukwa alisema Serikali iliamua kuanzisha Tuzo hizo kwa lengo la kutambua mchango wa Tasnia ya Filamu pamoja na kutambua vipaji vilivyojificha vya Wanatasnia ya Filamu.

"Tuzo hizi zilianzishwa kwa lengo la kuongeza hamasa ya Wanatasnia kuzalisha kazi nyingi zaidi za Filamu hivyo kuwepo kwa Tuzo hizi ni kuwapa moyo Sekta hii kuzalisha kazi zenye ushindani kufikia soko la Kimataifa," alisema.

Aidha alitaja vipengele vilivyowania tuzo hizo ambavyo ni Msanii Bora wa Kike Chaguo la Watazamaji, Wasanii waliofanikiwa kuingia ni Bi Stara kupitia Filamu ya Kombolela.

Wema Sepetu Filamu ya Malkia, Hidaya Njaidi Filamu ya Moyo, Thecla Mjata kupitia Filamu ya Nafu, Frola Mvungi kupitia Filamu ya Mwanahawa pamoja na Chuchu Hansy Filamu yake ya Beki Tatu.

Kipengele cha Msanii Bora wa Kiume Chaguo la Watazamaji waliofanikiwa kuingia katika kipengele hicho ni Nkwabi Ng'wanamala maarufu kama Mzee Kikala kupitia Filamu ya Kombolela.

Adam Nawanda kupitia Filamu ya *"Merchandizer",* Ayubu Bombwe Filamu ya "Alifu kwa Ujiti", John Kokolo kupitia Filamu ya "Wandongwa".

Ndumukwa alifafanua zaidi kuwa Wasanii waliofanikiwa kupita kwenye kinyang'anyiro hicho watatembelea vivutio vya utalii Mkoa wa Kilimanjaro na Jiji la Arusha kwa ujumla.

Pia alitoa wito kwa Wachekeshaji kutengeneza stori zenye muunganiko.

''Wachekeshaji bado ni wazuri, lakini hadithi au stori zao zinakosa muunganiko wa ule ucheshi kuzingatia maeneo ambayo wachekeshaji wazuri hawaonekani au kutokea basi kipande hicho kinakosa ucheshi," alisema.

Kwa upande Zamaradi Nzowa moja ya Waratibu wa Tuzo za Filamu alisema kura zitapigwa kwa njia mbili kupitia mfumo wa ujumbe mfupi pamoja na kupitia mfumo wa Tovuti ukiambatanisha na Code ya Msanii au kazi unayoipigia kura.

Nae Msanii Neema Walele alitoa pongezi kwa Waandaji wa Tuzo hizo kwa kuratibu zoezi la mchujo bila upendeleo wala kuangalia ukongwe kwenye Tasnia ya Filamu.

"Nipongeze zaidi Waratibu wa Tuzo hizi kazi yangu ndio ya kwanza kutengeneza lakini nilipoamua kuingiza kwenye mchakato huu nimefanikiwa japo katika mchuano huo vipengele nilivofanikiwa kuingia kuna wakali zaidi yangu ambao wamenitangulia katika Tasnia," alisema.

Aidha aliwaomba wadau wampigie kura kwa wingi ili waweze kumpa ushindi na kuendelea kutengeneza kazi nzuri zitakazoweza kuingia katika soko la Kimataifa na Mitandao mbalimbali ikiwemo *Netflix.*

Kwenye mwendelezo wa Tuzo hizi, bodi imedhamiria kuendelea kuendesha mchakato huu kila mwaka na kwa ubora tofauti ili kuwapa nguvu Wasanii ya kufanya kazi kwa kutumia maarifa na ubunifu mkubwa.

Ukitazama Filamu zetu zimefika kila kona ya Mikoa hapa nchini na zingine zinafanya vizuri kwenye Nchi jirani. Wito ni kwa kila Msanii kuhakikisha anafanya kazi kwa moyo ili kukuza na kujenga zaidi Tasnia hiyo.



SIKU YA KILELE CHA TUZO ZA FILAMU ARUSHA



MUIGIZAJI BORA MPAMBE WA KIKE
**SITI AMINA**



MUIGIZAJI BORA CHIPUKIZI WA KIUME
**COLLINS FRANK**

## KILELE CHA TAMASHA LA USIKU WA TUZO 2022

1. FILAMU BORA FUPI - **ATWE**
2. FILAMU BORA VIKARAGOSI - **KICHANGA**
3. MAKALA BORA - HADO - **HIFADHI ARDHI DODOMA**
4. FILAMU BORA UHARIRI - **OPERATION M22**
5. MUONGOZAJI BORA WA KIKE - **LEAH MWENDAMSEKE**
6. MUONGOZAJI BORA WA KIUME - **JUMA SAADA**
7. FILAMU BORA PICHA - **MALAIKA**
8. FILAMU BORA MZIKI - MOYO - **LODY MUSIC**
9. FILAMU BORA HAIBA - **VUTA N'KUVUTE**
10. FILAMU BORA MANDHARI - **VUTA N'KUVUTE**
11. FILAMU BORA USANIFU - **STILL OKAY TO DATE**
12. FILAMU BORA SAUTI - **OPERATION M22**
13. FILAMU BORA MAPAMBO ATHARI - **MAKEUP - MATEKA - JAFARI ATHUMANI**
14. MUSWADA BORA - **VUTA N'KUVUTE na WANDONGWA**
15. FILAMU BORA MAVAZI - **WANDONGWA**
16. MUIGIZAJI BORA WA KIUME - **NKWABI NG'WANAMALA - MZEE KIKALA**
17. MUIGIZAJI BORA WA KIKE - **TUNU MBEGU**
18. MUIGIZAJI BORA MPAMBE WA KIUME - **COJACK CHILO**
19. MUIGIZAJI BORA MPAMBE WA KIKE - **SITI AMINA**
20. MUIGIZAJI BORA CHIPUKIZI WA KIUME - **COLLINS FRANK**
21. MUIGIZAJI BORA CHIPUKIZI WA KIKE - **LIGHTNESS ROBERT**
22. TAMTHILIA BORA - **KOMBOLELA**
23. FILAMU BORA NDEFU - **VUTA N'KUVUTE**
24. FILAMU BORA UCHESHI - **USIPITE ENEO LA JESHI**
25. TAMTHILIA BORA UCHESHI - **JAMBO NA VIJAMBO**
26. MCHEKESHAJI BORA - **ABDALLAH NZUNDA (MKOJANI)**
27. FILAMU YA UELIMISHAJI WA MASUALA YA UKIMWI - **TIMIZA NDOTO**
28. FILAMU BORA YA KUTANGAZA UTAMADUNI - **KOMBE**
29. MUIGIZAJI BORA WA KIUME CHAGUO LA WATAZAMAJI - **JACOB STEPHEN - JB**
30. MUIGIZAJI BORA WA KIKE CHAGUO LA WATAZAMAJI - **WANSWEKULA ZACHARIA**





MUIGIZAJI BORA WA KIUME CHAGUO LA WATAZAMAJI
**JACOB STEPHEN**



MUIGIZAJI BORA WA KIKE
**TUNU MBEGU**

Tuzo mbalimbali za heshima zilitolewa kwa kutambua mchango wa Watunukiwa katika kuchangia maendeleo ya Sekta ya Filamu.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John Mongella, Aliyekuwa Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo Mhe. Mohamed Mchengerwa ambaye pia alikuwa mgeni rasmi katika kilele hicho.

Aidha, Bodi iliwatunuku Wanatasnia ya Filamu wengine 10 ambao kwa umahiri wao walisaidia kuinua Sekta ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Nchini kama ifuatavyo: -

**1. Yvonne Cherrie - Monalisa**
**2. Single Mtambalike - Richie Richie**
**3. Wema Sepetu - Wema**
**4. Jacob Stephene - JB**
**5. William Mtitu - Mtitu**
**6. Mahsein Awadhi - Dr. Cheni**
**7. Mussa Banzi**
**8. Raymond Allen - Bishanga**
**9. Vincent Kigosi - Ray**
**10. Theckla Mgaya – Aisha**

Tuzo tatu maalum zilitolewa kwa Washindi akiwemo NEEMA NDEPANYA aliyepokea Tuzo ya SPECIAL JURY AWARD kupitia Filamu ya MALKIA, Nguli wa Filamu nchini Marehemu STEVE KANUMBA alitunukiwa Tuzo ya Heshima kwa umahiri wake katika Tasnia ya Filamu.

Mkurugenzi Mtendaji wa ITV BI. JOYCE MHAVILE kwa mchango wake katika kuhakikisha Tasnia ya Filamu na Michezo ya Kuigiza inakuwa kwa kasi.



Kumbukumbu ya wadau wa Filamu katika vivutio vya Utalii kabla ya kuelekea Kilele cha usiku wa Tuzo za Filamu 2022.



Washindi mbalimbali wa Tuzo za Filamu kwa mwaka 2022.

# WASANII WANAOKUJA KWA KASI KATIKA TASNIA

## Said Zubeir (Kimbembe) BADO ANAPAMBANA NA HALI YAKE



KIMSINGI Tasnia ya Maigizo ya luninga kwa maana ya Tamthilia ndiyo namba moja kwa sasa nchini. Kimsingi biashara ya CD ni kama imeingia mchanga hapa kwetu.

Televisheni Mtandao *(YouTube),* zimekuwa kimbilio la Wasanii wengi sana, lakini pia baadhi ya Chaneli kubwa zinazomilikiwa na Azam TV, DSTV, Startimes na zingine zimekuwa uti wa mgongo wa Wasanii wengi.

Huko pia, kumeshuhudiwa pia Wasanii wengi wapya na wachanga wakizaliwa na kuibuliwa kila mwaka. Hususan kwenye kipindi cha miaka hii miwili hadi mitatu.

Kwa wale ambao wanatazama sana Azam TV Chaneli namba 103, watakuwa mashuhuda wa hili jambo. Kuna Wasanii wengi sana wameibuliwa huko na wanafanya vizuri sana.

Kati ya Wasanii hao ni Said Zubeir, ambaye alijizoelea umaarufu kupitia Tamthilia ya Mama Kimbo, akijulikana kwa jina la Kimbembe. Huyu jamaa ni moja kati ya majina ambayo yanakuja kwa kasi sana.

Hana miaka mingi kwenye gemu lakini amekamata macho, midomo na masikio ya watu wanaopenda Tamthilia zetu hapa nchini. Watoto wa Mjini, huwa wanatumia neno 'anajua'.

Kimbembe kwa sasa anafahamika kwa jina la Mbwana NangaNanga, jina ambalo linapendwa na Watazamaji wa Tamthilia ya Zahanati ya Kijiji inayorushwa na Azam TV.

Amecheza uhusika mgumu sana, ambao kwa macho ya kawaida unaona kama rahisi, yaani kutoka kuwa mmbea kwenye Saloon ya Mama Kimbo, hadi kuwa mtoto mwenye matatizo ya akili.

Tuachane na hayo, Kimbebe au Mbwana NangaNanga, tumepata nafasi ya kuzungumzana naye na amefunguka mambo machache kuhusu kazi na maisha yake. Hapa anaanza kwa kutupa historia yake.

"Jina langu ni Sad Zubeir, wengi wananifahamu kama Kimbembe na sasa Mbwana NangaNanga".

"Kwenye Tasnia nina miaka 6 ila mwaka ulionifanya nitambulike zaidi ni 2021, baada ya kushiriki Tamthilia ya Saluni ya Mama Kimbo".

"Tamthilia nilizowahi kushiriki ni "Mwantumu", "Saluni ya Mama Kimbo" na sasa nipo natamba na "Zahanati Ya Kijiji" ambayo kimsingi ndiyo habari ya mjini.

**Ni kwa kiasi gani unafurahia kazi yako ya Sanaa?**
"Kazi yangu ya sanaa naifurahia kwa kiasi kikubwa, maana imechukua nafasi kubwa katika maisha yangu".

**Changamoto unazokutana nazo kwenye kazi yako ya Sanaa ni zipi?**
"Changamoto zipo lakini ninachofahamu kila kazi ina changamoto zake, hivyo kwa upande wangu nazichukulia kama chachu ya kuniimarisha zaidi".

**Ni namna gani umekuwa Kioo cha jamii kama Msanii?**
"Changamoto ni za kawaida kwa sababu kwenye maisha ya kawaida tu yanakuwa na changamoto, kikubwa ni kuvumilia na kupambana bila kukata tamaa.

**Ni nani amekuwa Mshawishi wako mkuu katika Sanaa?**
"Wasanii wote wanaofanya vizuri, wa ndani na nje ya Nchi wamekua wakinijenga mimi kufanya vizuri zaidi sababu nimekua nikijifunza vingi kutoka kwao".

**Ni malengo gani umepania kuyatimiza maishani?**
"Malengo ni mengi ila kubwa kuwahakikishia Mashabiki zangu nitaendelea kuwapa burudani, mpaka pale Mwenyezi Mungu atakaponitoa kwenye uso wa Dunia".

**Mbali na Sanaa ni shughuli gani unajishuhulisha nazo Kiuchumi?**
"Nimekuwa nikifanya biashara zangu binafasi ambazo kimsingi zinasaidia kuniingizia kipato nje na kazi yangu ya Sanaa".

**Ni mafanikio gani umeyapata kwenye sanaa?**
"Allahmdulilah! Mafanikio ya kwanza ni kuwa na watu, sababu watu ndiyo wanaonifanya nizidi kukua na kung'ara kila siku".

"Hivyo nikisema nihesabu mafanikio cha kwanza kwangu kuwa na mashabiki wengi, kiasi kwamba kokote nikitokea basi itafahamika kuwa nipo. Mafanikio mengine yanabaki kuwa sehemu yangu binafsi zaidi.

## Asha Ali Chanzi (Bi Ubwa)
## MACHO YA WATU YANAMPA SHIDA MTAANI



KWA kipindi cha hapa katikati, Tasnia ya Filamu ilikumbana na ukata wa Wasanii Wanawake ambao wanaweza wakavaa na kucheza nafasi tofauti tofauti.

Zamani kidogo kulikuwa na watu kama Marehemu Mama Abdul, Bi Mwenda na wengine ambao ulikuwa ukiwapa kazi basi wanafanya zaidi ya vile ambavyo ulitaka iwe.

Wasanii kama Bi Chau, walikuwa wachache na bado hawajapatikana wengi, yaani unakuwa na mama fulani mwenye gubu, kero, vituko na kila aina ya hila.

Sasa kwa wale ambao wanatazama Zahanati Ya Kijiji kwa sasa, kuna burudani fulani wanaipata kutoka kwa Nesi Bi Ubwa, ambaye vituko na mambo yake ni burudani tosha kwa Watazamaji.

Pengine watu wengi inawezekana, wamemjua kuanzia pale kwenye Zahanati Ya Kijiji, lakini ukweli ni kwamba ni Msanii ambaye amefanya kazi nyingi sana ambazo hakuwahi kuharibu.

Hapa tupo na Bi Ubwa, ambaye kimsingi atazungumza kazi zake ambazo amefanya, changamoto na vitu ambavyo anaona na vinamsumbua Mtaani kutokana na kazi yake hiyo ya Uigizaji ambayo ameifanya kwa muda mrefu kidogo kwa sasa.

Hapa Bi Ubwa, anaanza kwa kutuambia kuwa yeye ni nani, amefanya kazi gani na amekutana na Wasanii gani kwenye kazi ambazo amewahi kuzifanya kipindi cha nyuma kabla ya Zahanati ya Kijiji.

"Jina langu ni Aisha Ali Chanzi, nina majina mengi maarufu kutokana na kazi ambazo zimefanya. Wapo wanaoniita Mama Kasikasi, lakini jina kubwa kwa sasa ni Bi Ubwa".

"Filamu ambazo nimecheza hadi sasa na nikafanya vizuri ni "Uwanja wa Dhambi" ya Haji Dilunga, "Danga Langu", "Shughuli ya Mwanangu", Ubunge ??? na Naoa Tena" zote zikiwa za Mkojani".

"Zingine ni "Kaja na Ngoma nikiwa na Bi Kauye", nimecheza Video au Filamu nyingi fupi nikiwa na Joti ambazo zilifanya vizuri sana pia".

"Nimeshiriki kwenye Tamthilia nyingi ambazo zilikuwa zinaruka Dstv, kama "Yalaiti", "Kidogo" na Tamthilia ya "Pazia" na sasa nipo "Zahanati Ya Kijiji".

**Ni kwa kiasi gani unafurahia kazi yako ya Sanaa?**
"Kwa kiasi ambacho hakielezeki nafurahia kazi yangu ya sanaa, napenda ninachokifanya na ndiyo maana nakosa kueleza ukubwa wa furaha ninayopata.

**Changamoto unazokutana nazo kwenye kazi yako ya Sanaa ni zipi?**
"Sina changamoto kubwa, nyingi za kawaida tu kwenye maisha ya kazi, ila kitu kinachonisumbua sana kwa sasa ni changamoto ya watu, wananishangaa sana kwahiyo macho ya watu ni mengi mno".

**Ni namna gani umekuwa kioo cha jamii kama Msanii?**
"Cha kwanza ni naburudisha watu nimekuwa miongoni mwa Wasanii ambao naburudisha Mashabiki zangu kwa kuwafurahisha pindi wanaponiona pia naelimisha jamii.

**Ni nani Amekuwa mshawishi wako mkuu katika Sanaa**
"Mume wangu ndio Mshawishi wangu mkubwa lakini mi mwenyewe napenda sana".

**Ni malengo gani umepania kuyatimiza maishani?**
"Malengo mengi na makubwa kwa mfano kufanya Tasnia yetu ya Filamu iweze kufika mbali ijulikane Dunia nzima.

"Pia kwa upande wangu natamani sana niweze kuwa Msaniii ama Mwanafilamu Duniani niweze kufanya kazi kubwa ndani na nje ya Nchi ama barani Afrika kwa ujumla.

**Mbali na Sanaa ni shughuli gani unajishuhulisha nazo kiuchumi?**
"Mbali na Sanaa najishughulisha na vitu mbalimbali, lakini pia ni Mfanyabiashara, Mchora piko, Mshereheshaji (MC), Ufumaji wa mashuka na vitu vingine vidogo".

**Ni mafanikio gani umeyapata kwenye Sanaa?**
"Bado sijapata mafanikio makubwa ila nashukuru Mungu riziki inapatikana ila sio sana ila naamini inanipa mafanikio tu".

## Collins Frank Ezekiel
## KANUMBA CHANZO CHA KUWA MWIGIZAJI



PALE Azam TV kuna Tamthilia inaitwa "Fungu Langu", ambayo inahusu zaidi mambo ya familia, wapo kina Jenifer Kyaka, Stanley Musungu, Chekibudi, Mayasa Mrisho na majina mengi makali.

Licha ya Tamthilia hiyo kuwa na majina makubwa, lakini kuna kijana mmoja anatumia jina la Nelson kwenye hiyo Tamthilia, anawasha sana moto.

Anaigiza na kufanya kazi kubwa sana na anaonekana kuwa na kipaji kikubwa sana cha kufanya Sanaa. Kijana huyo jina lake halisi ni Collins Frank Ezekiel akiwa na miaka 22. Yaani amezaliwa 2001.

Ana majina yake ya kazi kama Bestking na Acclaim. Tupo naye hapa kwenye hii Makala na anazungumza kuhusu maisha yake ya Sanaa.

**Ni kwa kiasi gani unafurahia kazi yako ya Sanaa?**
"Imekuwa kama ajira kwangu kwa sehemu kubwa sana na imekuwa kama utambulisho kwangu kwa jamii inayonizunguka".

**Changamoto unazokutana nazo kwenye kazi yako ya Sanaa ni zipi?**
"Wazazi wakati naanza walikuwa hawaamini kama ningeweza kufanya Sanaa wakati nasoma".

**Ni namna gani umekuwa Kioo cha jamii kama Msanii?**
"Sanaa kwa Wanafunzi wenzangu wamekuwa wakiomba niwashauri nini wafanye ili waweze kufika sehemu kupitia vipaji vyao wakiwa bado wanasoma".

**Una miaka mingapi kwenye sanaa?**
"Kwenye Sanaa kwa sasa nina mwaka mmoja.

**Ni nani amekuwa Mshawishi wako mkuu katika Sanaa?**
"Marehemu Steven Charles Kanumba, ndiye mtu ambaye kwa kiasi kikubwa kanifanya niwe Msanii".

**Ni malengo gani umepania kuyatimiza maishani?**
"Kufanya soko la Filamu kuwa kubwa Kimataifa na kuondoa dhana potofu walionayo wengi juu ya Tasnia ya Filamu".

**Mbali na Sanaa ni shughuli gani unajishuhulisha nazo Kiuchumi?**
"Ni mwanafunzi Shahada ya Sheria mwaka wa 3 katika Chuo kikuu cha Dar es salaam na pia ni Mjasiriamali".

**Ukuaji wa teknolojia kwenye Sanaa una msaada gani kwa upande wako?**
"Umenisaidia sana kukuza na kueneza kipaji changu kwa wengi ambao walikuwa hawanifahamu. Aidha inasaidia sana kufikisha na kusambaza kazi zangu nilizofanya kuwafikia watu wengi zaidi".

**Ni mafanikio gani umeyapata kwenye Sanaa?**
"Kushiriki katika majukwaa makubwa ya Sanaa. Kupata fursa nyingi za kazi za nje na ndani ya Nchi. Aidha kutimiza malengo yangu kupitia Sanaa.

**Umefanikiwa kuigiza filamu na thamthilia ngapi mpaka sasa na ipi imekupa jina?**
"Nimefanikiwa kupata nafasi ya kucheza Filamu mbili *"STILL OKAY TO DATE", "LOVE TRANSFUSION"*, kwa sasa natamba na Tamthilia "FUNGU LANGU na RIPOTI".

**Tuzo yoyote uliyowahi kuwania au kushinda?**
"Niliwania tuzo ya TAFFA kama Muigizaji Bora Chipukiza wa Kiume, SWAHILI WEEK FASHION kama *Best Fashion Content Creator*. Tuzo za EAESA kama Muigizaji Bora Chipukizi wa Kiume, na *UNIVERSITY AWARDS* kama Muigizaji Bora wa Kiume".

## Warda Seif
## JINA JIPYA KWENYE TASNIA YA FILAMU



Tasnia ya Filamu inashuhudia Mapinduzi ya wazi kutoka kwa Waigizaji mbalimbali Chipukizi ambapo mabadiliko haya huonekana kwa kasi kutokana na uwezo na ujuzi wa Waigizaji wapya wanaofanya vizuri katika Tasnia hii.

Katika Majina ya Wasanii wa Kike Chipukizi wanaofanya vizuri huku wakivaa uhusika tofauti tofauti huwezi kuacha kumtaja Warda Seif maarufu kama Salama jina ambalo alijizolea umaarufu kwenye Tamthilia ya Single Mama ya Jacob Steven almaaruf 'JB '.

Msanii huyo Chipukizi anaefanya vizuri kwa sasa Kipaji chake kilianza kuonekana mapema kunako miaka ya 2009 pale alipoanza kuonyesha umahiri wake wa Sanaa Shuleni akiwa darasa la 4.

Salama anasema kipaji chake kilianza kukaziwa nati na Msumari na Mjomba wake kutokana na kuvaa husika pasipo kuonesha aibu yoyote ile.

Warda Msanii ambae kwa sasa ana Miaka 24 akiwa Binti Mdogo 2010 alianza kucheza Filamu mbalimbali lakini hazikuweza kumtambulisha vizuri kwenye Kiwanda cha Bongo muvi.

Anamtaja Mkongwe wa Tasnia ya Filamu nchini Jacob Steven almaaruf 'JB' ndio aliye mshika mkono na kuwaonyesha Watanzania kuwa Warda ana Kipaji .

Tamthilia yake ya Kwanza ya"Single Mama" chini ya Jerusalem Film iliweza kuwaonyesha Watanzania kuwa Warda anaweza kuvaa uhusika vilivyo hasa alivyocheza kama Binti mdogo kutoka kwenye Familia ya kimasikini akiwa na tamaa na kujihusisha na mahusiano na watu waliomzidi umri.

Pia amepata nafasi ya kushiriki kwenye Tamthilia ya "Kombolela" pamoja na "Fundi".
Hata hivyo anatoa wito kwa Wasanii wakubwa kumpa nafasi kushirikiana nao katika kazi zao.
Anaeleza hisia zake kuwa anatamani kupata mtu ambae atamshika mkono ili afike mbali zaidi na kufanya kazi tofauti tofauti.

Anakiri kuwa Sanaa ndio kipaji chake na ndio ajira yake hivyo anatamani na anaongeza jithada ili aweze kuwania nafasi ya kuingia kwenye Tuzo za Filamu ili aweze kujipima uwezo wake na Wasanii wengine.

## Neema Walele (Brenda)
## ALIANZA KUIGIZA AKIWA DARASA LA PILI



NEEMA Walele siyo jina ngeni kwenye Tasnia ya Tamthilia na Filamu nchini, amekuwa akifanya kazi nyingi za kuigiza kwa miaka mingi.

Wengi wanamfahamu kwa jina la Brenda, leo tupo naye hapa na anazungumza na kutoa historia ya maisha na kazi yake.

Historia yako kwa ufupi
"Jina langu ni Neema Walele, nina miaka zaidi ya 30, nimezaliwa Dar ingawa mimi asili yangu ni Mnyamwezi kutoka Tabora na nimebahatika kuwa na watoto wawili.

"Kuhusu kuigiza nilianza nikiwa Shule ya Msingi huko Tabora ambako nilipata elimu yangu ya Msingi. Kipaji changu kiliibuliwa na Mwalimu wangu Levocatus Kimbelembele.

"Akanijenga na kunifunza njia zote za uigizaji, hapo ikanifanya nishiriki kwenye Mashindano ya UMITASHUTA tangu nikiwa darasa la pili na nikafanikiwa kuwa Muigizaji kinara kitaifa na hapo nikiwa darasa la tano.

"Kisha nikasimama, nikajikita zaidi kwenye masomo, baada ya masomo nikiwa na miaka kama 19 hivi nikarudi tena kwenye maigizo, ingawa kwa wakati huo nilikwa nashoot Matangazo tu.

Mwaka 2008, nikaigiza Filamu yangu ya kwanza inaitwa "Mtoto wa Mkimbizi". Kwahiyo safari yangu ikaanzia pale rasmi na nilipewa uhusika mkuu, baada ya hapo nikafanya kazi nyingi sana.

"Kwa sababu nilikuwa napenda kuigiza na kuonekana kwenye TV na nimefanya kazi bure sana kwa kuwa nilikuwa nataka kuwa maarufu".

**Changamoto unazokutana nazo kwenye kazi yako ya Sanaa ni zipi?**

"Changamoto siyo kubwa sana ni zile za kawaida tu, kama kuchelewa kurudi nyumbani, kukwazana na watu ambao unafanya nao kazi.

"Kukosa muda wa kukaa na watoto na kuwapa malezi yote kwa sababu kuna wakati unarudi nyumbani saa 9 Usiku na Asubuhi unaondoka tena. Labda kingine ni maslahi bado kusema unapata mzigo mkubwa".

**Ni namna gani umekuwa Kioo cha jamii kama Msanii?**
"Nimejaribu kuwavutia watu wengi sana kupenda Sanaa kwa sababu yangu mimi ukienda huko Mkoani. Mfano kwenye "Siri za Familia" ambako nimefaya kwa Episode 8 na jina la Brenda lilitokea huko.

"Baba yangu pia amekuwa shabiki mkubwa wa Sanaa kwa sababu yangu kwa kuwa mwanzo alikuwa haamini kupitia mimi. Lakini kwa sasa anajivunia kuona binti yake anafanya kazi hii ya Uigizaji.

**Una miaka mingapi kwenye Sanaa?**
"Kwenye Tasnia nina zaidi ya miaka 15, kwa sababu nilianza rasmi mwaka 2008. Nimefanya kazi nyingi sana, Tamthilia zaidi ya sita, Filamu zaidi ya 10".

"Hapo kuna "Ahadi", "Sinia", "Kosa Moja" na "Single Mama" ambayo watu wengi sana walinifahamu huko na kuna kazi nyingine nyingi ambazo zimetoka na hazijatoka".

**Ni nani amekuwa Mshawishi wako mkuu katika Sanaa?**
"Mimi napenda sana kuangalia kazi za nje, tangu nikiwa mdogo, lakini kwa hapa Tanzania navutiwa zaidi na 'Monalisa', ni dada angu, mtu mzuri na rafiki yangu pia.

"Amefanya kazi kwa muda mrefu sana lakini hana habari mbaya ni mtu ambaye ameweza kujificha kwa muda mrefu bila kuweka mambo yake hadharani licha ya kuwa mtu maarufu sana".

"Kwa Ulaya nampenda 'Angelina Jolie', ni mama na anafanya kazi ngumu na bado anabaki kuwa Mama na anaendesha maisha yake.

**Ni malengo gani umepania kuyatimiza maishani?**
"Nina ndoto kubwa sana, natamani kuona kazi zangu zikifika kwenye levo ya Kimataifa, kama *Netflix* huko, ingawa kuna vipande vichache vya "Binti" vilionekana huko lakini bado.

"Natamani kuwashika mkono na vijana wengine wenye vipaji huko na wao waweze kufikia malengo yao".

Mbali na Sanaa ni shughuli gani unajishuhulisha nazo Kiuchumi?
"Nafanya kazi nyingine ndogondogo kama ambavyo tunajua kuwa Sanaa yetu hailipi sana, licha ya kwamba imesaidia kusomesha wanangu, kuwa na kibanda changu, nina kigari kidogo. Lakini bado Sanaa haitupi tunachostahili.

**Ukuaji wa Teknolojia kwenye Sanaa una msaada gani kwa upande wako?**
"Umesaidia kurahisiha baadhi ya kazi zangu, kujitangaza na kupata kazi za kufanya".

## USHAURI WA RICH RICHIE KWA WASANII CHIPUKIZI



BILA shaka jina la Msanii Single Mohammed Mtambalike 'Rich Richie' halina ugeni masikioni mwa wapenzi, mashabiki na wadau wa Sanaa ya Maigizo, Tamthilia na Filamu kwa ujumla.

Hiyo inatokana na kuwa, Richie anayetaja siri ya mafanikio yake kuwa ni kuwa msikivu na kutojikweza kwa wengine, hususan mashabiki na wapenzi. Single 'Rich Richie' ni kati ya Wasanii Waanzilishi wa Michezo ya Kuigiza ya kwenye luninga.

Alianza kujipatia umaarufu mwaka 1997, alipokuwa akiigiza katika luninga ya ITV, akiwa na kundi lililokuwa likijulikana kama *'4 For You'*, lililojumuisha Wasanii 4, wengine 3 wakiwa ni Bishanga, Aisha na Waridi.

Richie anabainisha kuwa, akiwa na *'4 For You'* katika ITV, aliweza kushiriki kucheza michezo mingi iliyogusa nafsi za Mashabiki na Wapenzi mbalimbali.

"Mwaka 1998, tuliamua kubadili jina la kundi letu na kuliita 'Nyota Ensemble', baada ya kuliona limekwisha kuwa kubwa, ambapo tulishawaongeza pia Wasanii wengine kama JB, Monalisa na Natasha," anasema Richie.

Richie anasema, mwaka 2000, 'Nyota Ensemble' ilisambaratika, akaasisi kundi lingine lililotikisa vilivyo kwenye luninga ya CTN, lililojulikana kama 'Nyota Academia', akiwa na Wasanii zaidi ya 30, ambao wote wametokea kuwa maarufu mno hivi sasa.

Anawataja baadhi ya Wasanii hao kuwa ni Vicent Kigosi 'Ray', marehemu George Tyson, Lomole Matovolwa *'Big',* Abiola, Abdallah Kombora, Macklin Mdoe, Macha, Mjomba Fujo, Mobby Mpambala na Mack Legan Kipara wa Orijino Komedi.

Richie anasema kuwa, mwaka 2002, alianzisha kundi la 'Kamanda Family' lililowaibua wasanii kama Issa Mussa 'Claude', Shija, John Lista, Haji Adam 'Baba Haji', Hashim Kambi, John Kallage, Ahmed Olotu 'Mzee Chilo' na Fatma Shimweta.

"Ilipofika Juni, 2003, niliajiriwa na Kampuni ya kutengeneza majani ya chai, 'Chai Bora', hivyo nililiacha kundi la Kamanda mikononi mwa Baba Haji, nikaenda kuwajibika kama Meneja Masoko na Matangazo," anasema Richie.

Anasema kuwa, wakati huo alikuwa na Kampuni yake iitwayo 'Rich Richie *Art Promotion*' iliyokuwa na mkataba na Chai Bora tangu mwaka 2001, ambapo mwaka 2005, aliibadili jina Kampuni hiyo na kuiita 'Bulls Entertainment'.

Richie anaeleza kuwa, Kampuni ya Rich Richie ilikuwa ikijihusisha na matangazo pekee, lakini alipobadili jina na kuiita *'Bulls'* ikawa pia inajishughulisha na uandaaji filamu, kuuza na kukodisha wasanii na maonyesho.

Kadhalika, anasema kuwa, alikwishapata mafanikio mengi tangu ajitumbukize katika sanaa ya uigizaji. Kupitia kampuni yake ya Bulls ambapo, alipokea tenda kemkemu hizi na zile zilizomfanya awajibike kila uchao bila kupumzika.

"Nilionekana kwenye filamu nne kabambe, ikiwamo moja ya kwangu mwenyewe, 'Skendo', iliyotikisa sokoni niliyowashirikisha Rose Ndauka 'Mamaa wa Bulls', marehemu Adam Kuambiana, Dk. Cheni, Mobby Mpambala, Faiza Ally na Barafu," anasema Richie.

Anazitaja nyingine alizocheza akiwa ameshirikishwa kuwa ni 'Kimya', *'Perfect Man'* pamoja na 'Zawadi ya Birthday' inayoandaliwa na Kampuni ya Jerusalem Film Company, akicheza kama Daniel.

Baadhi ya filamu nyingine alizowahi kucheza miaka ya nyuma zaidi ni 'Agano la Urithi', 'Kwa Heshima ya Penzi', *'Copy'*, 'Kindergarten' pamoja na zile nne za kwake mwenyewe ambazo ni 'Solemba', 'Swahiba', 'Mahabuba' na 'Stranger'.

'Rich Richie', aliyezaliwa Oktoba 5, mwaka 1972, jijini Dar es Salaam na kubahatika kupata elimu ya msingi katika shule ya Mnazi Mmoja na ya Sekondari katika shule ya Al Hamain, zote jijini Dar es Salaam.

Ushauri kwa Wasanii Chipukizi
Richie amekuwa msanii mkubwa na mahili kutokana na kuongeza bidii katika kipaji chake na kusikiliza maelekezo ya watu mbalimbali.

Katika hilo ameamua kutumia fursa na jukwaa hili kuwapa ushauri vijana juu ya kile ambacho wanatakiwa kufanya ili waweze kutoboa kwenye kazi zao za Sanaa ambazo wanafanya.

"Wasanii wanapaswa kusikiliza ushauri kwa waliowatangulia, pia kuongeza ubunifu wao kwa sababu mtarishaji wa tamthilia anaangalia mtu mwenye vionjo vingi,".

Msanii huyo anasema kazi ya Sanaa ni kazi kama zingine hivyo vijana wanapaswa kutambua hilo na kuongeza bidii katika uigizaji.

"Tunahitaji kupata wakina Richie wengine katika Tasnia ya Uigizaji, vijana wanatakiwa kuongeza bidii katika kuigiza na kukubali kukosolewa."



# TAMTHILIA NA FILAMU
## ZINAZOTAMBA KWA SASA

TASNIA ya Tamthilia na Filamu kwa sasa imechangamka sana, kuna mchanganyiko wa kazi nyingi kutoka kwa Wakongwe na Vijana wenye damu changa.

Hiyo inafanya kila upande uwape hamasa upande mwingine kufanya kazi bora. Kwenye Visimbuzi huko kuna mpishano mkubwa wa kazi, kila mmoja akitaka kufanya kazi bora zaidi.

Hiyo imefanya tuone mabadiliko makubwa sana kwenye utendaji wa kazi hizo za Sanaa kuanzia stori, Uigizaji, Washiriki, mazingira hata namna ya kuongoza na kupiga picha za matukio.

Lakini kwenye uwingi huo wa kazi kwa maana ya Tamthilia na Filamu, sio zote ambazo zinakimbiza au kufanya vizuri, zipo ambazo zinafuatiliwa sana na nyingine kawaida tu.

Makala hii inakusogezea kwa uchache zile Tamthilia ambazo zinafanya vizuri na hata Filamu ambazo zimefika mbali na kutoboa Mtaani kwa ngazi ya Kitaifa na Kimataifa.

### FUNDI




Tamthilia ya "FUNDI" ilianza kutimua vumbi kwenye Kisimbuzi cha Azam TV kuanzia tarehe 7/11/2022 siku ya J3, ilikua inaruka kuanzia saa 1:30 usiku.

Muongozaji alikuwa ni Duma, ambaye pia alikuwa Mwigizaji Mkuu akiwa na Waigizaji wengine kama Shamsa Ford, Frola Mvungi na Mastaa wengine.

Tamthilia hii ilifanya vizuri sana mtaani, na ilimalizika takribani mwezi mmoja uliopita na kuacha kumbukumbu kwenye vichwa vya Wapenda Filamu na Tamthilia nchini.

### ZAHANATI YA KIJIJI




Inawezekana hii ndiyo ikawa Tamthilia pendwa zaidi nchini ambayo inaruka Azam TV, Zahanati Ya Kijiji ambayo ilianza takribani mwezi mmoja uliopita, imebeba hadithi tamu na inayopendwa sana Mtaani.

Uwepo wa waigizaji mchanganyiko, wakongwe na wapya kunanogesha zaidi tamthilia hiyo, uwepo wa Bi Star, Kimbembe, Tausi na Masala, Diku, Bi Ubwa, Mauja, Ombeni na Washiriki wengine.

Tamthilia hii imechezwa mkoani Lindi, ikiandikwa na Abdul Juma 'Writer', ikiongozwa na Director Majag, ni moja kati ya tamthilia pendwa sana

## FUNGU LANGU




Ukitaka kujua kama wenye familia kuna mambo mengi, basi tazama Fungu Langu, ni Tamthilia moja kali na pendwa ambayo inaruka kupitia Azam TV pia.

Jeniffer Kyaka, Stanley Musungu, Mayasa Mrisho, Chekibudi, Wasanii Chipukizi kama Loreen Khalfan, Collin Frank, Dolly Doche na wengine wameifanya Tamthilia hii kuwa moja kati ya zinazopedwa sana kwa sasa.

## KOSA MOJA

HII ni tamthilia ambayo inaruka Azam TV, kuna majina makubwa kwenye Tasnia ya Utangazaji na Uigizaji humo ndani, Mtu Imara na Salma Dakota kutoka Wasafi FM.

Wasanii wakongwe kama Cathy Rupia, Mau Fundi, Adam, wakichanganyikana na Wasanii Chipukizi kama Naah, imeifanya iwe kazi bora sana




## JUA KALI



Kutoka kwenye mikono ya Mwanadada Lamatah Leah, hapa hakuna namna nyingine ya kuweza kusimulia utamu na ubora wa kazi hii.

Quick Rocka, Mimi Mars, Lulu Diva, Stanley Musungu, Romy Jones, na wakali wengine kama Gabo, Dorah hawa wote wanafanya kazi isonge mbele na kwenda juu zaidi.

Achilia mbali uwepo wa waigizaji kutoka nje ya Nchi. Inaruka kupita Kisimbuzi cha DSTV.

## HUBA




Hii ipo kwenye mikono salama ya gwiji wa Filamu na Tamthilia nchini Jacob Stephen 'JB', halafu humo ndani kuna gwiji mwingine Mwanamama Grace Mapunda.

Binti machachari Jenifer Kanumba, Mr Pimbi, Ramy Galis, Mbotto, Nandy, Tino, Nicole, Carlos, Ben Kinyaiya, Esha Buheti, Nelly Kimwelu, Fabrizo na majina mengine ambayo wanaiweka juu Tamthilia hii inayoruka DSTV.

## KOSA MOJA

Hii ni Tamthilia mpya ambayo inaruka Azam TV, ambayo ipo chini ya Chuchu Hansy, akiwapa mashavu Mastaa kama Ray Kigosi, Rich Mtambalike, Thea, Lukamba na wakali wengine ambao wanaifanya iwe kati ya Tamthilia kali Bongo.




## KITIMTIM




Hii ni tamthilia ya Vichekesho ambayo inarushwa DSTV, humo ndani wapo kina Tin White, Mkono wa Mkonole, Masantula, Ringo, Sabufa, Dullvan na wengine na kuifanya iwe bora.

# WAPAMBAJI

## (MAKE UP ARTISTS

### NA KAZI YA KULETA UHALISIA KATIKA FILAMU

Ukizungumzia Mapambo *(Make-Ups)* watu wengi akili huenda moja kwa moja kwenye kupendeza, lakini ukizungumzia Wapambaji *(Make Up Artists)* unazungumzia kitu tofauti kabisa.

Katika Filamu huwa kunakuwa na uhusika tofautitofauti, watu huweza kucheza kama Mke wa mtu, Sugar mummy, Changudoa, House Girl, Chizi, Jini, Mchawi n.k.

Na kama unavyojua kwamba Filamu ni kuchukua maisha halisi na kuyaweka katika maigizo hivyo ni muhimu kumfanya mtu anaecheza sehemu fulani afananie na sehemu anayocheza.

Hufanyika hivyo ili aweze kuleta uhalisia kwa maana ya kuvaa uhusika kamili siyo wa maneno tu bali hata muonekano, kama ni Chizi inabidi aonekane Chizi kweli, kama ni Changudoa muonekano wake inabidi uwe hivyo.

Na hiyo ni kulingana na sehemu anayocheza na si kwa kupendeza peke yake kama ambavyo wengi tunafikiria.

Hivyo maana halisi ya Mapambo athari *(Make-ups)* katika Filamu ni kitu chochote ama ile hali ya kumbadilisha mtu ili aweze kuwa na muonekano na afanane kwenye uhusika anaotakiwa kuucheza.

Kwenye sehemu husika inaweza ikawa wa kupendeza ama kuchukiza. mfano mtu anaweza akacheza kama Mzimu ama Jini, mhusika anaweza akapakwa masizi.

Kwenye Filamu hata kama mtu amepakwa masizi ili atishe, hiyo kwenye Filamu hatutaita masizi bali ni Mapambo athari (Make-Ups). Na hivyo ndivyo Mapambo athari (*Make Ups)* yanafanya kazi kwenye shughuli za Filamu na Tamthilia.

Lakini tukirudi kwenye Filamu zetu za hapa nyumbani, mara nyingi Wapambaji *(Make-Up Artists)* wetu wanashindwa kwenye hili na sielewi tatizo linakuwa wapi, mtu anaweza akacheza yuko na ametoka kuamka lakini atarembwa kupitiliza kiasi kwamba hata ule uhalisia huupati ama yuko Kijijini hajawahi kufika hata Mjini na maisha yake ni ya hali ya chini kabisa lakini kawekwa dawa ama mawimbi *(Wave).*

Sasa swali la kujiuliza hapa hivi haya Mapambo *(Make-ups)* yetu ni sawa kweli? zinaendana na mazingira halisi? Licha ya kuwa kuna mabadiliko makubwa ya Filamu na Tamthilia kutokana na ukuaji wa Teknolojia?

### TULIPO SASA

Ulimwengu wa urembo unazidi kukua karibu kila mwanamke kwa sasa anajua kujipamba na wengine wasiojua basi wanapambwa na wale wanaojua.

Kufanya mambo kuwa rahisi basi wale Wapambaji *(Make-up artists)* wanaojua huwa wanafundisha kupamba kwa darasa inaweza kuwa kwa mwezi au wiki inategemea na muda na mipango ya Mwalimu huyo.

Kutokana na ili tukajiuliza Je? hawa walimu wanajua mtu anataka kuwa makeup artist wa aina gani? Hawa wanafunzi huwa wanachukua muda wao kutaka kujua zaidi kuhusu Mapambo (Makeups) au ni kwenda na wakati kwa sababu biashara hii inalipa kwa sasa basi na wewe ufanye?

Sisi kwetu Wapambaji *(Makeup Artists)* ni Sanaa, unaweza kujifunza ukafanya lakini usiweke nguvu kubwa kama yule ambae anafanya kwa kupenda na sio kwa ajili ya kwenda na wakati.

Hii ndio utakuta wengi wanafanya kitu kimoja hamna utofauti wa kazi, lakini wale ambao huwa wanafanya kwa upendo huwa wanajaribu vitu vingine mara kwa mara.

Kuna aina nyingi za Wapambaji *(Makeup Artists)* lakini leo tunakuletea hizi 4 ambazo ndizo zinazojulikana sana.

**MPAMBAJI WA MITINDO *(FASHION MAKEUP ARTIST)***
Hawa ni wale ambao wapo nyuma ya maonesho mbalimbali ya sanaa, wapo nyuma ya kurasa za jarida.

Ili kuwa Mpambaji inabidi uwe unajihusisha na kujua nini kiko sokoni katika Uliwengu wa mitindo yaani mavazi na mapambo hii inasaidia kufanya kazi yako kuwa rahisi.

Lakini pia inabidi ujifunze namna ambavyo wanafanya kazi na uwe mbunifu kuwa na njia zako ambazo umezitengeneza mwenyewe.

**MPAMBAJI WA VIPODOZI *(BEAUTY MAKEUP ARTIST)***
Hawa ndio ambao tunao wengi, hawa wanafanya Mapambo ***(Make ups)*** kila siku za kawaida labda kwenye harusi, Red Carpet lakini pia huwa wanafanya vitu vingine kama kutengeneza nywele na uso 'facial treatment'.

Hawa ni wale Wapambaji ambao kwa hapa kwetu tunawaita Wapambaji wa Saluni (Saloon Makeup Artists) wawe wamesomea Veta, Makeup College au kwa mtu ila wanawaze kukupamba kutoka ulivyozoeleka kuwa vingine.



**PICHA MBALIMBALI ZA MAPAMBO *(MAKE UPS)* ZILIZOLETA UTOFAUTI NA UHALISIA**

**FILAMU - MPIGAJI**



**TAMTHILIA - JUA KALI**



**TAMTHILIA - KITIMTIM**



**TAMTHILIA - ZAHANATI YA KIJIJI**



**TAMTHILIA - HUBA**



**MPAMBAJI ATHARI WA FILAMU NA SINEMA *(FILM AND MOVIES MAKE UP ARTIST)***
Hawa ni wale ambao uwapaka Mastaa na kuwabadilisha muonekano katika Filamu na Tamthilia, kama ukiangalia Filamu za wenzetu kuna wale ambao wanapakwa Mapambo athari *(Special effects)* ya vidonda.

Wanambadilisha mtu kuonekana kijana au mzee, anaweza kubadilisha muonekano wa mwili n.k, hawa wanafanya zaidi kwenye Sinema na Filamu zile zenye stori ya kutisha, Uchawi na Mazombi.

Kabla ya kuingia huku ni vyema kujua unataka kuwa Mpambaji wa aina gani, hii itasaidia kupata mgawanyiko wa kazi lakini pia kupata ladha tofauti.

Tupende kujifunza na kujua zaidi kuhusu vitu tunavyotaka kufanya, hii itasaidia kuchagua kile ambacho ni bora.

Kwa sasa kazi za muziki na filamu zina tumia sana makeup artist lakini kwa bahati mbaya wale wangi tulionao wachache ndio wanajua kutofautisha Mapambo ya kawaida na Mapambo katika Filamu na Muziki.

# USHIRIKIANO
## WA WASANII
### WA KIMATAIFA KATIKA FILAMU ZETU NA TIJA YAKE

UHALISIA ni kwamba kwenye kazi ya Sanaa inapotokea Taifa moja limeshirikiana na Wasanii kutoka kwenye Taifa lingine lengo kuu huwa ni moja tu, ambalo ni kupanua wigo wa kibiashara.

Kwa sababu, kama Mtanzania atafanya kazi na Msanii kutoka Nigeria, moja kwa moja itakwenda kumfanya atambulike na kutengeneza soko kwenye Nchi ya Nigeria kupitia kazi hiyo.

Mifano ya hilo ipo mingi sana, kwani mwanzoni mwa miaka ya 2010, Marehemu Steven Kanumba aliweza kufungua milango ya Sanaa yake kwenye Taifa la Nigeria, mara baada ya kufanya Filamu ya Dar to Lagos ambayo walishirikiana na Wasanii wenye majina makubwa pale Nigeria.

Kisha zikafuatia kazi nyingine nyingi ambazo Kanumba alifanya na Wasanii kutoka Nigeria ambao aliwasafirisha na kuwaleta hapa. Baadaye Kanumba akafanya kazi na Staa wa Nigeria Van Vicker kwenye Filamu ya Devil Kingdom ambayo ilikuwa kali sana.





Celestine Gachuhi



Sho Madjozi

Kwa siku za hivi karibuni tumeona katika Tanthilia ya Jua Kali watu mbalimbali akiwemo Van Vicker, Richard Mofe, wakiwika Bongo kutoka Nigeria, Rabby Bray kutoka Ghana, Gloria Songoro kutoka Kenya, Shomadjozi kutoka South Afrika pia wakiwemo Celistine Gachuhi maarufu kama Selina katika tamthilia ya Yalaiti, Peter Kamau Tamthilia ya Jua Kali na Waigizaji wengine ambao wamekuwa wakifanya kazi kwenye Tasnia ya Kitanzania lakini pia kuna Wasanii wengi wa Tanzania ambao wanafanya kazi ya Tamthilia nchini Kenya.

Haya yote yamekuwa na tija kwa kuwa yanapasua anga na kutengeneza wigo mpana kwa Wasanii na Waigizaji kufanya vizuri katika anga la Kimataifa.

Lakini pia lengo la kuwapa mashavu wasanii ni kutaka kujikuza kwenye Mataifa mengine ambayo ni ngumu kupata soko lake.


Kulingana na tafiti mbalimbali za masuala ya Filamu Barani Afrika, Tasnia ya Filamu nchini Tanzania kwa sasa inashika nafasi ya tatu kwa kutoa filamu nyingi na ambazo zimekuwa zikitamba ndani na nje ya Bara la Afrika.

Vyuo vikuu mbalimbali Duniani vinavyotoa kozi ya lugha ya Kiswahili vimekuwa vikitumia Filamu za Kitanzania kujifunzia lugha hiyo kwa ufasaha.

Hata hivyo, bodi ya Filamu kupitia Wizara ya Sanaa na utamaduni imeweza kutoa mkopo kwa wasanii mbalimbali ikiwa ni chachu ya kuboresha na kusaidia katika kutoa kazi zilizo na uweredi na ubunifu.



Pascal Tokodi



Richard Mofe

# KONA YA MASHABIKI

## JUU YA KAZI ZA WASANII AMBAO WANAZIPENDA

Kazi yoyote ya Sanaa inafanywa na watu, watu hao wanafanya kwa ajili ya watu au kundi fulani la watu.

Inaaminika kuwa, maoni au mawazo yana nafasi kuu mbili, kujenga na kubomoa. Kuna watu au mtu ukimkosoa unakuwa umemuharibu kabisa.

Kuna ambao ukiwakosoa unakuwa umewajenga. Sasa hapa hii ni kona ya mashabiki ambao wamefunguka na kutoa maoni yao juu ya kazi mbalimbali za filamu na tamthilia wanazozipenda

**Director Tony**
“Mimi ni Mtangazaji wa radio na pia ni mdau mkubwa sana wa kazi za Filamu na Tamthilia. Napenda kazi nyingi za Wasanii kwa kuwa nimekuwa nikifanya nao kazi”.

“Kitu ambacho napenda kwenye kazi nyingi ni ubora wa utendaji kazi kwa maana ya video kuwa na ubora kwenye kazi nyingi. Ingawa bado kuna changamoto kubwa kwenye kupata watu sahihi wenye vipaji”.

**Hope Baby**
“Kitaaluma mimi ni Mfasihi (Literature), nimeandika vitabu vingi pale Chuo Kikuu cha Dar es salaam na kuandaa kazi nyingi.
“Tamthilia nyingi nzuri, mfano Jua Kali, Lamatah amejitahidi sana kuandika na kuongoza, kuna mambo mengi sana ambayo yanavutia kuyatazma”.

“Waigizaji wanabadilika kulingana na wakati, Muigizaji habaki na uhusika ule ule tu. Utakuta leo katili, kesho mtu mzuri na kuna mchakato wa kuona mabadiliko yake.

**Khadija Designer**
“Mimi ni mdau haswa wa Tamthilia na Filamu, napenda “Huba”, “Jua Kali” na kazi nyingine, kitu ambacho wanatakiwa kuboresha zaidi ni stori zao”.
“Nyingi zinakuwa nyepesi na rahisi kujua nini kinakwenda kutokea kesho. Kitu kingine wanatakiwa kutafuta sura ngeni ambazo zenye uwezo mkubwa na siyo kuwapa nafasi Wakongwe tuu ambao wengi wanaigiza kawaida.

**Zanura Shaibu**
“Mimi ni Mama wa nyumbani, lakini ni mdau mkubwa sana wa Tamthilia na Filamu, hakuna Filamu au Tamthilia kali ambayo sijaiona. Kwa sasa napenda zaidi “Zahanati ya Kijiji”.

“Mule ndani watu wote wameweza kuzishika vema nafasi zao. Ukimtazama Bi Ubwa, Diku na wengine wanacheza vizuri sana. Kitu pekee ambacho kinapunguW ni ushirikishwaji wa wanakijiji”.

“Inatakiwa kungekuwa na Scene mpito nyingi za wanakijiji kile ili kuongeza uhalisia, lakini wanajitahidi sana.

**Rashid Omary**
“Mimi ni Mwandishi na ukweli navutiwa sana na “Jua Kali”, nampenda sana Quick Rocka ameweza sana kubadilika mle ndani na kucheza uhalisia”.

“Alikuwa katili na Msela asiyejali wala kuwa na huruma kwa Wanawake, lakini unaweza kuona mapenzi yamemkamata na sasa analia tu kama Fala”.

**Mohamed Hussein**
“Mimi ni Digital Content Creator nipo East Africa TV, kuna shida binafasi naiona kwenye Tasnia yetu, hakuna Wasanii wapya wanaozaliwa na kuwa Mastaa, ukijiuliza tangu Kanumba amekufa ni Staa gani kazaliwa ambaye anashtuaTasnia, Madirector na Maproducer wenye nguvu wajikite kutengeneza stori ambazo kimsingi zitazalisha watu wapya.

“Lakini siyo mbaya kuna dogo anaitwa Frank Collins anacheza “Fungu Langu”, naona anakuja vizuri na anafanya vizuri. Namfuatilia sana”.

**Khadija Bakari**
“Nafikiri kwangu “Jua Kali” ni bora kwangu, napenda sana namna ambavyo Mimi Mars anacheza kwa uongo ambao upo kweli kwenye maisha ya Wasichana wengi wa mjini.
“Lamatah aongeze watu na Mastaa wengine kutoka nje nafikiri itazidi kumpa soko zaidi la Kimataifa.

**Juma Kakunda**
“Mimi ni mdau haswa wa Tamthilia na Filamu, napenda “Huba Series, lakini pia kuna ile Filamu ya “Binti” ya Seko Shamte, ni nzuri sana inatoa fundisho kubwa sana kwa Mabinti Zetu.
“Kibongobongo namkubali sana Grace Mapunda, ambaye anacheza “Huba” kama Tessy, anajua sana yule Mama, ukimuweka popote lazima akupe kitu.


**Anthony Makombo**
“Mimi nampenda sana Bi Star, yule Mama anajua sana kuigiza, ukimuona alivyocheza kwenye “Jua Kali”, ni tofauti kabisa na kwenye “Zahanati ya Kijiji”.

“Yaani kama Soka basi yule ni kiungo kama Sure Boy unampa mbaya yeye anakurudishia nzuri. Nafikiri Wwaandaaji wa hizi Filamu na Tamthilia wamzingatie sana yule Mama, anajua sana na huwa anaongeza kitu kwenye kazi”.

“Nyingi zinakuwa nyepesi na rahisi kujua nini kinakwenda kutokea kesho. Kitu kingine wanatakiwa kutafuta sura ngeni ambazo zina uwezo mkubwa na siyo kuwapa nafasi wakongwe tu ambao wengi wanacheza kawaida”.

**Zalina Mbarouk**
“Binafsi napenda Tamthilia ya “Jua Kali” na Mwigizaji ninayempenda ni Lucas, anajua sana kuigiza yuke Mkaka. Cha kuongeza kwenye Filamu zetu na Tamthilia ni ubunifu tu”.

# CHANZO NA HISTORIA YA MAJINA



## MUHOGO MCHUNGU

HIVI unajua kuwa kwa asilimia zaidi ya 90, Wasanii wote maarufu duniani wanatambulika kwa majina ambayo siyo yao ya kuzaliwa.

Ndiyo wengi sana, mfano Silvester Stallone, dunia nzima inamfahamu kama Rambo. Wapo wengi sana, nimemchukua huyo kama mfano tu.

Ukija kwa hapa Tanzania, ndiyo wengi sana wanatambulika kwa majina ambayo siyo yao. Vicent Kigosi (Ray), Othuman Njaidi (Patrick Kanumba) na wengine wengi.

Inawezekana kabisa, wewe ni kati ya mamilioni ya Watanzania ambao wanajua na kufahamu kuwa, Mzee Muhogo Mchungu, hili jina kazaliwa nalo.

Lakini ukweli ni kwamba hili ni jina ambalo linampa tu ugali na limetokana na kazi yake ya Sanaa, yaani Muhogo Mchungu siyo jina lake kabisa.

## SASA ANAITWA NANI?

Jina lake halisi ambalo alipewa na Wazazi wake baada ya kuzaliwa ni Mohamed Mkumbila. Na ukitazama asili ya jina la Mkumbila utagundua kuwa ni watu kutoka ukanda wa Kusini ambako ndiyo asili yake.

## MUHOGO MCHUNGU LILITOKEA HAPA

Kwenye mahojiano na Muhogo Mchungu, hakusita kuweka wazi kuwa jina hili alilipata siyo kwa makusudio yake, bali ni watu na shughuli zake ambazo alikuwa anazifanya.

Anasema ilikuwa ni miaka ya 80, ndipo alipopata jina hili na chanzo kikiwa na biashara zake ndogo ndogo ambazo alikuwa anazifanya, ikiwemo kuuza mihogo, ndizi, viazi na vitu vingine vya kula.

“Niliwahi kufanya biashara siyo kubwa sana, nilikuwa nauza mihogo, viazi na ndizi. Sasa ilitokea watu wakawa wanakuja wanasema muhogo huu mchungu”.

“Sasa ikawa ni kama kawaida, sasa nami nikaona hapa dawa ni watu kwenda nao hivi hivi, watu wakija kuuliza nikawa nawaambia muhogo huu mchungu”.

“Hapo ikawa mwanzo na jina likawa limepata nguvu zaidi na hadi sasa na ikabidi nilitumie hata kwenye kazi zangu za Sanaa”.

### AMITABH BACHCHAN ALIMFANYA AIGIZE

Muhogo Mchungu anasema yeye aliyemfanya awe Mwigizaji ni nguli wa India, Amitabh Bachchan, ambaye alikuwa akimtazama na kumfuatilia tangu akiwa kijana.

“Amitabh Bachchan, ndiye aliyenifanya niwe Mwigizaji na niingie kwenye Sanaa, nilikuwa napenda sana namna ambavyo alikuwa anacheza”.

“Nikaanza kutamani na mimi kutaka kufanya kama ambavyo yeye alikuwa anafanya. Hapo ikawa mwanzo wa kuanza kutafuta namna nzuri za kuweza kufanikiwa kufanya maigizo na nikatoboa”.



### ALIACHA KAZI YA AFYA KISA UIGIZAJI

Muhogo Mchungu anasema mwaka 1992 aliachana na kazi ya katika Hospitali ya Muhimbili kwa sababu ya kufanya Sanaa.

Kilichofanya aache kazi ya kuajiriwa ni kero ya kukosa kuhudhuria mazoezi ya vikundi vya Sanaa. Na aliacha kazi ambayo ilikuwa inamlipa vizuri ili kutimiza ndoto zake za kufanya Sanaa.

### CHANGAMOTO ALIYOWAHI KUKUTANA NAYO NI HII

“Changamoto ambayo nilikumbana nayo ni mzozo wangu na Mume wa dada mmoja ambaye alikuwa anawasiliana na mimi kwa lengo la kutaka kumsaidia kufanya kazi ya Sanaa.

“Kwa bahati mbaya mume wa yule dada akapata hisia tofauti na zile namna ambazo sisi tulikuwa tunawasiliana, nashukuru Mungu akaja akaelewa baadae kuwa hapakuwa na kitu kingine zaidi ya Sinema”.

### ASICHOPENDA KWA VIJANA WA SASA

“Hakuna kitu ninakichukia kama maisha ya kuigiza kwenye Mitandao ya Kijamii.

“Ninayachukia kwa sababu ipo siku mtu atakuja kuona maisha yangu halisi ashangae hivyo inapaswa kila mmoja kuishi vile Mungu amempangia na siyo kuigiza, hayo maisha feki tuyatupe kule.




# BODI YA FILAMU TANZANIA

***Filamu ni Biashara, Filamu ni Ajira***


**Barabara ya kivukoni**
Utumishi, kitalu H,
S.L.P. 79241,
DAR ES SALAAM

+255 222 121 920
+255 222 121 921

**www.filmboard.go.tz**


---